

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**BUNGE LA TANZANIA**

---

**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA  
BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA  
KUANZIA MACHI, 2018 HADI JANUARI 2019**

---

*[Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za  
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

Ofisi ya Bunge,  
S.L.P. 941,  
**DODOMA**

**FEBRUARI, 2019**

## YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA.....	1
1.0 MAELEZO YA JUMLA.....	1
1.1 Utangulizi .....	1
1.2 Majukumu ya Kamati .....	1
1.3 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati.....	2
SEHEMU YA PILI .....	3
2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI.....	3
2.1 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI .....	3
2.2 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO .....	4
2.2.1 Mradi Na. 6260 SIDO Institutional Support.....	5
2.2.2 Ziara katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu .....	7
2.2.3 Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Mgodu wa Wachimbaji Wadogo Sekenke One - Singida.....	8
2.2.4 Ziara ya Kamati kwa Wadau wa Sekta ya Viwanda .....	10
2.3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 .....	17
2.3.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 .....	17
2.3.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Ofisi ya makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.....	21
2.4 TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE ...	24
2.5 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE .....	53
SEHEMU YA TATU .....	73
3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO .....	73
3.1 Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.....	73
3.1.1 Upokeaji wa Fedha kutoka Hazina .....	73
3.1.2 Mradi wa Chuma wa Liganga na Mradi wa Makaa ya mawe wa Mchuchuma .....	73
3.1.3 Mradi wa Kufufua Kiwanda Cha General Tyre .....	74
3.1.4 Shirika la Maendeleo la Taifa – NDC .....	74
3.1.5 Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo - SIDO.....	75
3.1.6 Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo Wa Udhhibiti Wa Biashara Nchini .....	75

3.1.7	Mazingira ya Kufanyia Biashara Nchini .....	76
3.1.8	Uwepo wa Bidhaa Feki Sokoni, .....	76
3.1.9	Viwanda Vilivyobinafsishwa .....	<b>Error! Bookmark not defined.</b>
3.1.10	Vibali vya kuingiza Sukari Nchini.....	77
3.2	Usimamizai wa Mazingira .....	<b>Error! Bookmark not defined.</b>
3.2.1	Changamoto za Baraza Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira .....	77
3.2.2	Ufinyu wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira.....	77
3.2.3	Tozo za Mazingira kuingizwa katika Mfuko wa Mazingira .....	78
SEHEMU YA NNE.....		79
4.0	HITIMISHO.....	79

**TAARIFA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU  
YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KWA KIPINDI  
CHA KUENZIA MACHI, 2018 HADI JANUARI, 2019**

*[Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za  
Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika** kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira naomba kuwasilisha taarifa inayoeleza shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2018 hadi Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu Nne ambapo, Sehemu ya Kwanza inaelezea Utangulizi, Sehemu ya Pili inaelezea namna Kamati imetekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha kuanzia Machi 2018, hadi Januari, 2019 na matokeo yaliyobainishwa, Sehemu ya Tatu inaelezea Maoni na Mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

**1.2 Majukumu ya Kamati**

Kwa mujibu wa Fasili ya 6 (1) ya Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inajukumu la kusimamia shughuli za Sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira. Kwa muktadha huo na kwa kuzingatia matakwa ya Fasihi ya 7(1) ya Nyongeza ya Naane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Kamati hii inatekeleza majukumu yafuatayo:-

- (i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji, na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;

- (ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara hizo;
- (iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara hizo; na
- (iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hizo.

### **1.3 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kuisimamia na kuishauri Serikali Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilitumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

- (i) Kupokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji za Wizara na taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati; Taarifa hizi zilijumuisha taarifa za kawaida za utekelezaji wa majukumu ya wizara na taarifa za utekelezaji wa bajeti za wizara ambapo Kamati ilizipokea, kuzichambua na kuzijadili na hatimaye kuishauri Serikali kadiri Kamati ilivyoona inafaa;
- (ii) Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya ziara katika miradi mbalimbali kwa lengo la kubaini ufanisi uliopo katika kutekeleza Miradi hiyo;
- (iii) Vikao na wadau wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Kamati iliwatembelea pamoja na kuwaalika wadau hao mbele ya Kamati kwa lengo la kufahamu namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanikio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha;
- (iv) Kamati ilihudhuria semina mbalimbali zilizoendeshwa na wadau wa sekta za Viwanda, Biashara, Uwekezaji na Mazingira wa lengo la kuwajengea wajumbe uelewa juu ya sekta hizo.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2018 na Januari, 2019 Kamati iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni katika kuzisimamia Wizara zake mbili (2) na Taasisi zilizopo chini yake.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu yaliyotekelezwa na Kamati ni pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zinazoripoti kwa Kamati; Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa mwaka unaoishia pamoja na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka unaofuata; na Vikao na wadau wa Sekta zinazosimamiwa na Kamati kwa lengo la kusikiliza maoni yao; na kuhudhuria Semina za kujenga uelewa wa Wajumbe.

### 2.1 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wizara ya Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Kamati ilitoa ushauri kwenye maeneo mbalimbali. Serikali imejitahidi kuzingatia ushauri huo, hata hivyo kuna baadhi ya ushauri ambao Kamati imeona kuwa hayajatekelezwa ipasavyo. Maeneo ambayo Kamati imeona ushauri wake haukutekelezwa ni haya yafuatayo:-

i) Kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Uwekezaji, Kamati iliitaka Serikali kufanya yafuatayo:-

***a) Kupeleka fedha zilizosalia kwa ajili ya mradi wa TAMCO ili uweze kukamilika kwa wakati kama ilivyopangwa. Pia itekeleze miradi ya aina katika maeneo mengine ya uwekezaji yaliyotengwa katika sehemu mbalimbali nchi.***

***b) Kuongeza kasi ya uwekezaji wa miundombinu wezeshi katika Mradi wa Industrial Park Kibaha.***

***c) Kuongeza kasi ya utekelzaji wa Mradi wa General Tyre kwa vile kukamilika kwake kutaongeza mchango katika Pato la Taifa lakini kuongeza ajira pia.***

ii) Kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Kamati iliitaka Serikali kufanya yafuatayo;-

***a) Kuangalia upya Sheria za Misituzi, Mazingira na Mifugo ili kuondoa mgongano wa kisheria katika utekelezaji na uhamasishaji wa usimamizi wa Mazingira. Mazingira ni suala mtambuka na usimamizi wake unazigusa Wizara na Sheria tajwa hivyo ni vema zifanyekazi pamoja.***

***b) Tozo zinazotokana na shughuli zinazochangia uharibifu wa Mazingira ni nyingi lakini zinakusanywa na Taasisi au Idara nyingine za Serikali. Kamati inashauri tozo hizo walau kwa asilimia 5 ziingie katika mfuko wa Mazingira. Mfano tozo ya magari chakavu, tozo ya mkaa, tozo ya mafuta na tozo ya magogo.***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliarifiwa hatua mbalimbali za utekelezaji wa ushauri huo lakini haikuridhishwa na hatua hizo. Kamati inaishauri Serikalil kuongeza kasi ya kutekeleleza ushauri huo.

## **2.2 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara za ukaguzi wa ufanisi uliopo katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama inavyoelekezwa na kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha kuanzia tarehe 14 hadi 19 Machi, 2018 Kamati ilitembelea miradil mitatu (3) inayotekelezwa na Wizara ya Viwanda,

Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Miradi hiyo ni Mradi Na. 6260 – *SIDO Institutional Support* Mkoani Iringa, Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu – Mkoani Iringa na Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Mgodini wa Wachimbaji Wadogo wa Sekenke One Mkoani Singida.

### **2.2.1 Mradi Na. 6260 SIDO Institutional Support**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembela **Mradi Na. 6260 -** *SIDO Institutional Support*, Mradi huu unatekelezwa nchi nzima lakini Kamati ilipata fursa ya kutembelea karakana ya SIDO-Iringa (kituo cha uendelezaji wa Teknolojia Iringa) na kujionea jinsi wanavyoendesha shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika,** karakana ya SIDO – Iringa inaendesha shughuli za kubuni na kutengeneza mitambo mbalimbali ambayo hutumiwa na wajasiriamali katika kurahisisha shughuli zao za uzalishaji. Pamoja na kutengeneza mitambo hiyo, kituo kinaendesha mafunzo na kutoa ushauri kwa wajasiriamali kuhusu uzalishaji na matengenezo endelevu kwenye mitambo wanayowauza.

**Mheshimiwa Spika,** karakana ya SIDO - Iringa inakabiliwa na changamoto ya matumizi ya mitambo ya zamani (tangu miaka ya 1970) ambayo inapelekea kuwepo matumizi makubwa ya umeme na kusababisha bidhaa wanazozalisha kuuzwa kwa bei kubwa ikilinganishwa na washindani wao. Pia uchakavu wa mitambo unaosababisha kazi nyingi kufanyika kwa mikono hivyo kutumia muda mwingi kwa uzalishaji usio na tija.

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine ni upungufu mkubwa wa watumishi (Karakana inawafanyakazi watatu (3) tu) hivyo kupelekea fundi mmoja kufanya kazi zaidi ya uwezo wake; pia miundombinu mibovu katika eneo la SIDO - Iringa jambo linalopunguza ufanisi wa kituo.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto hizo bado karakana ya SIDO-Iringa imefanikiwa kubuni na kutengeneza mitambo mbalimbali ikiwepo



mtambo wa kusafishia mafuta ya Alizeti-Double refinery uliofungwa CHATO AMCOS Mjini Chato, mtambo wa upepo na mvuke wa kukaushia chai kwa kiwanda cha Chai cha Kisogo, mtambo wa kusindika zao la Kakao na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali vya ufundi.

### **Maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Institutional Support-SIDO Iringa**

**Mheshimiwa Spika**, SIDO ni taasisi nyeti na muhimu sana katika kutekeleza azma ya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa viwanda kwa kutengeneza vipuri kwa ajili ya viwanda vingine. Kamati inaishauri Serikali kuwa;-

- i) Kuwezesha Taasisi ya SIDO kikamilifu ili iweze kufufua karakana zake zote nchini;
- ii) Kuiwezesha SIDO kubuni teknolojia rahisi itakayo zalisha mashine na mitambo inayoendana na uhitaji wa soko; na
- iii) Kuajiri watumishi wenye weledi katika fani mbalimbali zinazohitajika katika karakana za SIDO.

**Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya SIDO kupitia mfuko wa NEDF huwasidia wajasiriamali kwa kuwakopesha mitaji. Serikali imekuwa ikitenga bajeti ndogo isiyoendana na mahitaji halisi ya huduma za mfuko jambo linalopelekea kukwamisha ufanisi wa Mfuko. Kamati inaendelea kuishauri Serikali;-

- i) Kuongeza bajeti ya Mfuko wa NEDF, ili kuiwezesha kuwiana na mahitaji halisi. Hatua hii itauwezesha mfuko kuwafikia wananchi wengi zaidi, lakini pia itawezesha kutoa mikopo mikubwa zaidi kwa wajasiriamali tofauti na ilivyo sasa kiasi cha juu cha mkopo ni shilingi Million Tano (5,000,000); na
- ii) Fedha zinazopitishwa kwa ajili ya NEDF zipelekwe kwa wakati ili kuweza kutekeleza majukumu lililokusudiwa.

### 2.2.2 Ziara katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inatekeleza Mradi wa Usimamizi wa Ikolojia ya eneo la Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kurejesha mtiririko wa maji kwa kipindi cha mwaka mzima. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Bonde la Mto Ruaha Mkuu kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika Bonde na kujua mikakati ya Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira zilizojitokeza katika eneo la Bonde.

**Mheshimiwa Spika**, Bonde lote la Mto Ruaha Mkuu linajumuisha vyanzo vya mito mikuu Tisa (9). Kwa ujumla hali ya Bonde siyo ya kuridhisha na lipo katika **hatari ya kukauka** ndiyo maana **Mheshimiwa Makamu wa Rais**, aliamua kuiagiza Ofisi yake Idara ya Mazingira kuunda kikosi kazi cha kuhakikisha mto Ruaha unarudi katika hali yake ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Bonde la Mto Ruaha Mkuu linakabiliwa na chanagamoto zifuatazo;-

- i) Jamii kuendesha shughuli za kilimo katika maeneo ya Bonde hivyo kusababisha uchepushaji mkubwa wa maji pasipo kuzingatia mahitaji ya watumiaji wengine hasa wakulima wa Mpunga Mbarali;
- ii) Ongezeko kubwa la idadi ya mifugo inayochungwa katika eneo la hifadhi;
- iii) Kupanuka kwa shughuli za binadamu hasa kilimo cha mpunga katika mashamba ya Mbarali na kulima kando ya mikondo ya mito; na
- iv) Kukinzana kwa baadhi ya Sheria katika kusimamia uhifadhi wa Bonde la Mto Ruaha Mkuu (Sheria ya Mita 60 na Sheria za usimamizi wa Mabonde chini ya Wizara ya Maji)

**Mheshimiwa Spika**, katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu, Kamati iliweza kubaini kubaini changamoto na kutoa ushauri kama ifuatavyo;-

- i) Bonde la Mto Ruaha linatumiwa na wadau mbalimbali, mfano shughuli za Uhifadhi wa wanyama (Ruaha National Park), uvuvi, kilimo na ufugaji hali inayopelekea Bonde hili kuelemea. Ili kupunguza madhara ya uchepushaji na upotevu mkubwa wa maji unaotokana na kutozingatia kanuni za Mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa Elimu ya matumizi sahihi ya maji hasa kwa jamii zinazoendesha shughuli zake katika eneo la Bonde; na
- ii) Waendeshaji wa miradi mikubwa ya uzalishaji umeme ambayo inategemea maji kutoka katika Bonde hili (Bwawa la Mtera, Kidatu na Mradi mpya wa *Stieglers Gorge*) watambue uhusiano mkubwa kati ya miradi yao na uhifadhi wa mazingira katika Bonde la Mto Ruaha Mkuu. Itumike busara ya Miradi hiyo ya Umeme kuchangia katika kuhifadhi wa mazingira ya Bonde kwa uhai wa miradi yao.

### **2.2.3 Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Maeneo ya Mgodi wa Wachimbaji Wadogo Sekenke One – Singida**

**Mheshimiwa Spika**, shughuli mbalimbali za binadamu zimekuwa zikiendesha bila kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, miongoni mwa shughuli hizo ni uchimbaji madini. Utekelezaji wa Sheria za Mazingira katika migodi nchini bado siyo wakuridhisha, kwa mujibu wa kaguzi zilizofanyika hadi kufikia Disemba, 2017 kati ya **migodi 128** ni **migodi 5** tu sawa na **asilimia 4** ndiyo inayozingatia Sheria za Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa pia ya kutembelea mgodi wa wachimbaji wadogo wa Sekenke One Mkoani Singida kwa lengo la kujionea namna wanavyoendesha uchimbaji, hali ya mazingira katika eneo la mgodi na uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika eneo la mgodi.

**Mheshimiwa Spika**, hali ya mazingira katika eneo la mgodi sio ya kuridhisha, Kamati ilijionea mambo yafuatayo;-

- i) Wachimbaji wadogo wakitumia kemikali hatari ya zebaki katika Kuchenjua dhahabu bila kuwa na vifaa vya kujikinga, kitendo hiki kinaathiri mazingira lakini pia afya za wachimbaji hao na jamii inayoishi eneo linalozunguka mgodi;
- ii) Matumizi ya teknolojia duni ikiwemo matumizi ya magogo katika kuzuia kingo za mashimo/migodi na kusababisha ukataji wa miti katika maeneo mengi nchini; na
- iii) Uchimbaji wa kubahatisha bila kuwa na uhakika wa kiasi cha madini kilichopo ardhini hivyo kunasababisha kuwepo na mashimo mengi ardhini.

**Mheshimiwa Spika,** katika mgodi wa Wachimbaji wadogo la Sekenke-One Kamati ilibaini changamoto nyingi na tukatoa ushauri katika mambo yafuatayo;-

- i) Ili kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa misitu hovywa kwa ajili ya kupata magogo yanayotumika katika zoezi la uchimbaji. Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake za ufundi kubuni njia mbadala ambayo itakuwa rafiki kwa mazingira na afya kwa wachimbaji wadogo. Mfano badala ya kutumia magogo wanaweza kutumia chuma;
- ii) Wachimbaji wadogo nchini wanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mitaji na hivyo kulazimika kutumia zana duni na kusababisha athari kubwa za mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuwasiliana na taasisi za fedha zinazoweza kuwakopesha fedha au vifaa kwa riba nafuu;
- iii) Wachimbaji wadogo wanatumia teknolojia duni katika uchimbaji na uchenjuaji, jambo linalopelekea kiasi kikubwa cha Dhahabu kubaki katika makinikia mwisho wa siku wanakuwa wametumia nguvu nyingi kuwanufaisha watu wengine (wachimbaji wadogo wanapata asilimia **30** tu na asilimia **70** inabaki kwenye makinikia ambayo wanauziwa wenye mitambo ya kuchenjulia).

Kamati inaishauri Serikali iangalie namna ya kuwasaidia ili kuongeza tija kwa wachimbaji wadogo na kuongeza mapato kwa Serikali.

**Mhesimiwa Spika**, wajumbe walihoji kuhusu matumizi ya Zebaki katika uchenjuaji kwa wachimbaji wadogo, Wizara yenye dhamana ya kusimamia mazingira iliirifu Kamati kuwa Serikali ipo katika mpango wa kutekeleza Mkataba wa *Minamata Convention* wenye lengo la kupunguza matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini ili kupunguza madhara ya kemikali hii kwa afya za binadamu na mazingira kwa ujumla. Kamati inapongeza kwa jitihada hizo na inaendelea kuisisitiza Serikali iharakishe utekelezaji wa mpango huo kwa lengo la kuokoa maisha ya wachimbaji na jamii zinazoishi kuzunguka maeneo ya migodi.

#### **2.2.4 Ziara ya Kamati kwa Wadau wa Sekta ya Viwanda**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea viwanda vitatu vinavyozalisha bidhaa za Mabati, Nondo na Mabomba, viwanda hivyo ni pamoja na kiwanda cha ALAF LTD ambao wanazalisha mabati, kenchi za chuma, masufuria na sahani za chuma; kiwanda cha MM Industries LTD ambao wanazalisha bidhaa za mabati, nondo, bomba za chuma, gypsum na matanki ya plasiki; na kiwanda cha Lodhia Steel Industries LTD wanaozalisha nondo, mabomba ya chuma, mabomba ya plastiki na matanki ya plastiki.

**Mheshimiwa Spika**, viwanda hivi vinakabiliwa na changamoto ya uwepo wa bidhaa za mabati na nondo nyingi sokoni zinazouzwa bei ndogo ikilinganishwa na bidhaa wanazotengeneza wao. Kinachopelekea hili ni pamoja na:-

- a) Uagizwaji wa bidhaa zisizokidhi viwango kutoka nje ya nchi hususani mabati na kuuzwa bei ya chini ikilinganishwa na bei za mabati yanayozalishwa nchini.
- b) Ukwepaji kodi (*under declaration of tax liability*) hali inayopelekea kuuzwa bei ya chini sokoni. Wafanyabiashara wasiowaaminifu kwa

kushirikiana na watendaji wasio waaminifu hushirikiana kuingiza mabati ambayo hupitia hatua zote za uzalishaji na kuyatoza kodi kama mabati ghafi (*semi processed*).

- c) Wakandarasi wanaotekeleza miradi mikubwa ya nchi ikiwepo miradi ya maji kutumia vifaa ambavyo huagizwa kutoka nje ya nchi wakati viwanda vyetu vina uwezo wa kuzalisha malighafi hiyo.

**i) Viwanda vya vinywaji baridi na Vinywaji vikali**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipata fursa ya kutembelea viwanda vya vinywaji baridi ambapo ilitembelea kiwanda cha Coca Cola Kwanza ambao ni wazalishaji wa vinywaji baridi aina ya Coca Cola, Fanta, Mirinda na juice za matunda mbalimbali; kiwanda cha Bakhresa Food Products Mkuranga ambacho huzalisha juice za aina mbalimbali. Kwa upande wa vinywaji vikali Kamati ilitembelea Kiwanda cha Tanzania Breweries LTD (TBL) na Kiwanda cha Serengeti Breweries LTD (SBL) ambao ni watengenezaji na wasambazaji wa vinywaji vikali kama bia na pombe kali. Viwanda vinavyotengeneza vinywaji baridi na vikali vinakabiliwa na changamoto zifuatazo;-

**a) Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%)**

Serikali iliongeza ushuru wa forodha kwa 15% kwa waagizaji wa Sukari ya viwandani nchini ili kuwadhibiti wafanyabiashara wasio waaminifu. Ushuru huu unapaswa kurejeshwa kwa wenye viwanda baada ya kuwasilisha matumizi TRA na kuhakikiwa.

**Mheshimiwa Spika,** tunatambua na kukubaliana na nia nzuri ya Serikali ya kuwadhibiti wafanyabiashara wasiowaaminifu lakini utekelezaji wake umegeuka kuwa ni kero. Takribani miaka mitatu sasa tangu utaratibu huu kuanzishwa, Serikali imeshindwa kurejesha fedha hizo.

**b) Ushuru wa Stampu ya Kielekroniki (*Electronic Tax Stamp*)**

Katika Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilipitishwa kodi ya ushuru wa stampu (*Electronic Tax Stamp*), kwa ajili ya kuwadhibiti wamiliki wa viwanda

wasio waaminifu wanaotoa taarifa za uwongo za uzalishaji na kulipa kodi kidogo.

**Mheshimiwa Spika**, mfumo uliopendekezwa na Serikali katika kukusanya kodi hiyo ni ghali mno, mfano wazalishaji wa Soda, bia na juice, sigara na pombe kali kodi kwa stempu moja ni kati ya shilling 8 mpaka 49, kiasi hicho ni kikubwa kuliko kodi ambayo inalipwa Serikalini. Aidha, Kiasi hicho kitalipwa kwa wakala wa mfumo na si Serikali.

**c) Uwepo kwa pombe kali (spirits) bandia sokoni**

Uwepo wa pombe kali bandia sokoni ambazo hutengenezwa katika maeneo mbalimbali yasiyo rasmi na kuuzwa kwa bei ya chini kuliko zinazotengenezwa na viwanda vyetu na kupelekea kuua soko la bidhaa zinazozalishwa hapa nchini na kulipa kodi Serikalini.

**d) Ongezeko la Kodi kwenye Pombe kali aina ya Valuer**

Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali iliogeza kodi katika pombe kali aina ya Valuer kutoka shilingi 200 mpaka shilingi 3215 kwa lita hivyo kuikosesha ushindani katika soko. Pombe hii ilikuwa inatengezwa na Kiwanda cha Bia Tanzania (TBL) ambacho kilisitisha uzalishaji wa bidhaa hii baada ya kukosa ushindani kwenye soko. TBL walikuwa wanunuzi wakubwa wa zabibu kwa ajili ya kuzalisha Valuer, kuanguka kwa bidhaa sokoni kutaleta athari kubwa kwa wakulima wa zao hili.

**ii) Kiwanda cha Sigara Tanzania (TCC Ltd)**

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilipata fursa ya kutembelea kiwanda cha kutengeneza sigara, kiwanda hiki kinazalisha aina mbalimbali za sigara kwa kutumia tumbaku.

**Mheshimiwa Spika**, wamiliki wa kiwanda hiki wanalalamikia kuwepo kwa Kodi ya Stampu ya Kielektroniki jambo linalopelekea gharama za uzalishaji kuwa kubwa na na kupelekea kuongeza bei ya bidhaa zao. Aidha, uwepo wa Kodi ya Stampu ya Kielektroniki kutaongeza ugumu katika kupanga bei mpya ya sigara mfano, kwenye mzunguko wa fedha hakuna shilingi 15/=, 20/=,

25/= n k. Sambamba na hilo wanalalamikia ugumu wa mazingira ya kufanya biashara nchini jambo linalopelekea kuendelea kufungwa kwa biashara nchini na kushuka kwa mauzo.

**iii) Kiwanda cha mafuta ya kula cha Murza Wilma**

**Mheshimiwa Spika,** wamiliki wa kiwanda hiki wanalalamikia ongezeko la kodi katika mafuta ghafi yaingiayo kutoka nje kutoka asilimia 10 mpaka asilimia 25. Ongezeko hili la kodi limesababisha uingizaji wa mafuta hayo kwa njia za panya kuwa mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** nia ya Serikali kuongeza kodi hii ili kuvilinda viwanda vya ndani ni njema sana lakini haitafanikiwa kwa kuwa wafanyabiashara wasio waaminifu wanaendelea kuingiza mafuta kwa njia za panya na mafuta hayo yataendelea kuuzwa kwa bei ya chini kuliko yanayozalishwa nchini. Kamati inaishauri Serikali kujitahidi kudhibiti mipaka yetu pamoja na bandari bubu kwa lengo la kuzuia uingizaji mafuta usio rasmi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ziara hii Kamati iliona kuna haja ya kuwaalika wadau wengine wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji chini ya Jumuiya ya Wafanyabiashara Wenyeviwanda Tanzania (CTI) mbela ya Kamati ili kuwasikiliza maoni yao juu ya mazingira ya biashara nchini lengo likiwa ni kupata maoni ya wadau wengi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** wadau waliofika mbele ya Kamati waliwasilisha changamoto zilizofanana na zile zilizowasilishwa na wenye viwanda wakati wa ziara ya Kamati. Wadau hao waliongezea baadhi ya changamoto ambazo ni pamoja na;-

- a) Kukinzana kwa Sheria zinazosimamia Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji,** Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji zinasimamiwa wa Mamlaka mbalimbali za udhibiti. Mamlaka hizi zimeanzishwa kisheria lakini Sheria zinazoziongoza mamlaka hizo zimeonekana kukinzana na mazingira halisi ya sasa ya biashara.



- b) Ukubwa wa Gharama za uzalishaji,** Wadau wamelalamikia gharama za uzalishaji nchini ni kubwa jambo linapelekea bei ya bidhaa zinazozalishwa kuwa kubwa kuliko zile zinazolingia kutoka nje, hivyo kushindwa kushindana katika soko.
- c) Ugumu wa Upatikanaji wa Vibali vya kuingiza sukari ghafi nchini,** Upatikanaji wa vibali hivi umegubikwa na urasimu sana jambo linalosababisha baadhi ya Viwanda kusitisha uzalishaji kwa muda na vingine kufikiria kufunga viwanda.
- d) Mawasiliano hafifu kati ya mamlaka mbalimbali za Serikali,** Utendaji wa Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji unahusiana na maamuzi Wizara nyingine kama wizara ya Ardhi kupata vibali vya ardhi, Wizara ya Nishati kupata umeme, Wizara ya Maji kupata huduma ya maji, Mamlaka ya Uhamiaji kupata Vibali vya kuingia nchini, Wizara ya Fedha katika kodi na tozo mbalimbali. Changamoto iliyopo ni Mamlaka hizi kutofanya kazi kwa pamoja jambo linalokwamisha utekelezaji wa shughuli za viwanda, biashara na uwekezaji.

**Maoni na Ushauri wa Kamati juu ya Hoja za Wadau wa Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji:**

**a) Kodi ya Kieletroniki ya Ushuru wa Stamp:**

**Mhesimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na nia nzuri ya Serikali kuhusu kuanzishwa kwa kodi ya ushuru wa stampu ili kuwadhhibiti wazalishaji wasio waaminifu, lakini Kamati ina maoni na ushauri ufuatao;

- i) Utekelezaji wa kodi hii utapelekea kupandisha bei na kusababisha kupungua kwa mauzo kwa kiasi kikubwa hali inayoweza kusababisha kupunguzwa wafanyakazi na kupungua mapato ya Serikali kutoakana mishahara (PE) na kodi ya mapato (*Business Income*);
- ii) Mfumo wa ETS kama unavyopendekezwa na Serikali ni ghali sana. Wadau wapo tayari kushirikiana na Serikali ili kubuni mfumo mwingine kwa gharama nafuu kwa manufaa ya pande zote ni vema Serikali ikakaa na kushauria na wadau hawa;

- iii) Utekelezaji wa kodi hii utawalazimu wenye viwanda kuongeza bei ya kila bidhaa kwa Shilingi 100/= kwa sababu Sarafu nyingine hazipo kwenye mzunguko hivyo kuzifanya kushindwa kushindana katika soko.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaikumbusha Serikali kuwa, wajibu wa msingi wa wafanabiashara ni kulipa kodi lakini gharama za ukusanyaji wa kodi ni za Serikali. Utekelezaji wa Mfumo huu wa kodi utawalazimu wadau kuweka miundombinu ya ukusanyaji wa kodi ambalo si jukumu lao, Kamati inaishauri Serikali kuzingatia haya.

**Mheshimiwa Spika**, kuna baadhi ya Viwanda ambavyo vilitakiwa kuwa mfano kwa kuanza kutekeleza mfumo huu wa kodi, viwanda hivyo ni viwanda vinavyozalisha pombe kali na viwanda vya Sigara. Viwanda hivyo vimekwisha anza utekelezaji wa agizo hili, takribani mitambo 37 imekwishafungwa katika viwanda mbalimbali na changamoto zilizohisiwa kuambatana na mfumo huo wamekutana nazo ikiwemo changamoto ya kupunguza kasi ya mitambo ya uzalishaji (*slow down production*)

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa viwanda hivi vilitumika kama mfano, Kamati inaishauri Serikali kuwatembelea wenye viwanda hivyo na kushauriana nao kwa lengo la kuboresha kabla ya mfumo huu kuanza kutumiwa na wadau wote.

#### **b) Ushuru wa Forodha 15% (refundable import duty 15%)**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali bado haijarejesha kiasi kikubwa cha tozo hii kwa wenye viwanda wanaotumia Sukari ghafi nchini jambo linalopelekea viwanda hivyo kushindwa kujiendesha kutokana sehemu kubwa ya mitaji yao ipo Serikalini. Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo;

- i) Kurejesha fedha hizo kwa wakati kwa kuwa nyingi ni mikopo kutoka katika taasisi za fedha hivyo kusababisha malimbikizo ya riba na marejesho. Aidha, viwanda hivi vinashindwa kujiendesha kutokana na kiasi kikubwa cha mitaji yao kuwa Serikali, hali hii ikiendelea watalazimika kusitisha uzalishaji.

- ii) Kwa kuwa utekelezaji wa mfumo huu umeonekana kuwa kero, Serikali iuondoe na badala yake ipendekeze adhabu kwa wote watakaodhihirika kufanya udanganyifu;

**Mheshimiwa Spika**, bado kuna urasimu unaochelewesha upatikanaji wa vibali vya kuagiza sukari ghafi nchini, hivyo kusababisha viwanda kuzalisha kwa msimu. Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali hivyo kwa wakati na kwa wale wanaofanya udanganyifu wachukuliwe hatua stahiki.

**c) Kuhusu kuwepo kwa bidhaa bandia za Bati na Nondo Sokoni:**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali iongeze udhibiti katika Bandari zake hususani Dar es Salaam kwa kuimarisha ukaguzi wa bidhaa za Bati na Nondo kutoka nje ya nchi;

**Mheshimiwa Spika**, mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu jambo ambalo halitoi taswira nzuri kwa ustawi wa wawekezaji nchini. Kamati inaishauri Serikali itafute kiini cha tatizo hili ili kujenga imani kwa wawekezaji;

**Mheshimiwa Spika**, aidha, wakati wa kuingia makubaliano ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa fedha za misaada au mikopo ya masharti nafuu, Serikali ijitahidi kuweka vifungu/utaratibu ambao utawaelekeza wakandarasi wanaopewa kazi kununua mahitaji yao kutoka ndani ya nchi mfano, mabomba, nondo, bati n k. Hatua hii itasaidia kuchochea ukuaji wa viwanda na kulinda ajira za ndani bila kuathiri suala ubora. Utaratibu wa sasa wa kununua bidhaa hizo kutoka nje unawanufaisha zaidi wageni na kutoa ajira nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kupunguza kodi ya pombe kali aina ya valuer, ambayo hutengenezwa kutokana na matunda ya mizabibu, kwa lengo la kusaidia wakulima kuwa na soko la Zabibu la uhakika na kuchochea ukuaji wa kilimo hicho nchini hasa hapa Dododma ambapo Mheshimiwa Spika wapiga kura wako ni wakulima wazuri za Zabibu;

## **2.3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati za Bunge za Kisekta hufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoishia na kufanya ulinganisho wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha unaofuata. Jukumu hili limeainishwa katika Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

### **2.1.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Katika kufanya uchambuzi huu, Kamati ilizingatia makusanyo ya maduhuli, fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Chanzo cha taarifa hizi ni taarifa zilizowasilishwa na Wizara mbele ya Kamati na majadiliano yaliyofanyika na hatimaye kupata taarifa hizi muhimu.

#### **a) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa Fungu 44 na 60**

##### **i) Makusanyo ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na taasisi zilizopo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **28,000,000,000** kutoka katika makusanyo ya ada za leseni, mauzo ya nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara. Hadi kufikia kufikia Desemba, 2017 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **8,598,083,500.07** kiasi ambacho ni sawa na asilimia **30.7** tu ya lengo lililo kusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa, Desemba, 2017, takribani miezi sita (6), ya utekelezaji kwa mwaka 2017/2018, ni asilimia 30.7 tu ya lengo ndio ilikuwa imekusanya, jambo linaloashiria uwezekano mdogo sana wa kufikia lengo lililokusudiwa. Kamati iliishauri Serikali kupanga bajeti ya makusanyo maduhuli kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyake vya mapato ili kuwa na uhakika wa kufikia malengo.

ii) **Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2017/2018**, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji ilitengewa na kuidhinishiwa jumla ya shilingi **122,215,109,750.00** kati ya fedha hizo Shilingi **80,190,377,000.00** ikiwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Shilingi **42,024,732,750.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yake yote mawili **Fungu 44** Viwanda na **Fungu 60** Biashara na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Fungu **44** Viwanda lilitengewa shilingi **98,012,870,000.00** Kati ya fedha hizo Shilingi **73,840,377,000.00** zilikuwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **24,172,493,000.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Na Fungu **60** Biashara na Uwekezaji lilitengewa Shilingi **24,202,239,750.00**, kati ya hizo Shilingi **17,852,239,750.00** ni Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **6,350,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

iii) **Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa, hadi kufikia Machi, 2018, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **37,447,911,373.33** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na taasisi zilizopo chini yake. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **30.64** tu ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya mafungu yote **44** na **60**. Kamati ina maoni

kwamba, kuchelewa kutolewa kwa wakati fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kumekuwa kikwanzo kikubwa katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini mambo yafuatayo;-

- Asilimia kubwa ya fedha zilizopokelewa kutoka Hazina zilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, (Shilingi **29,447,911,373.33** ambazo ni asilimia **78.6** ya fedha zote zilizopokelewa zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengine) ambapo pia asilimia kubwa ya fedha hizo zilikuwa kwa ajili ya Mishahara. Mwenendo huu wa utoaji wa fedha kutoka Hazina unaashiria kuwa hakuna uwiano wa upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida na fedha za Miradi ya Maendeleo;
- Hadi kufikia mwezi Machi, 2018, kati ya Shilingi **80,190,377,000.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi bilioni **8** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa kwa mafungu yote mawili **44** na **60** kutoka bajeti ya Fedha za Ndani, kiasi hiki ni sawa na asilimia **9.97** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo. Hali hii imekwamisha utekelezaji wa miradi mingi kwa wakati hali inayopelekea kupanda kwa gharama mwaka hadi mwaka; na
- Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kiwango kikubwa unaonyesha kuwa Serikali inapanga matumizi makubwa yasiyoakisi uhalisia wa vyanzo vya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina umekuwa siyo wakuridhisha, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha inapeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## **b) Makisio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha unaoishi Kamati hufanya ulinganisho wa Makisio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata kwa lengo la kupata uhalisia wa kiasi kinachoombwa ukilinganisha na utekelezaji wa mwaka ulioisha katika kipengele cha ukusanyaji wa Maduhuli na kipengele cha maombi ya fedha.

### **i) Makisio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imepanga kukusanya Shilingi **20,006,300,000.00** kwa **Fungu 44 na 60** kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni, leseni za biashara, faini kutokana na kukiuka masharti ya leseni pamoja na marejesho mishahara endapo mtumishi ataacha kazi.

Kiasi hiki ni pungufu kwa asililimia **28.5** ya Shilingi **28,000,000,000.00** kiasi kilichokadiriwa katika ya Mwaka wa Fedha **2017/2018**. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia ushauri wa Kamati wa kujikadiriwa kwa kuzingatia uwezo wao halisi wa Makusanyo.

### **ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mafungu yote Mawili (Fungu **44** na **60**) ilitengewa Shilingi **143,334,153,648.00**. Kiasi hiki ni zaidi kwa asilimia **17.28** ya shilingi **122,215,109,750.00** ya bajeti iliyotekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Kati ya fedha zinazoombwa, Shilingi **43,309,628,648.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **100,024,525,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka (ongezeko la asilimia **17.28**) ambalo ni jambo jema na la kupongezwa. Changamoto inakuja katika upatikanaji wa fedha hizo kutoka Hazina ambao si wakuridhisha mfano halisi ni bajeti ya mwaka 2017/2018 hadi kufikia Machi, 2018 ni asilimia **30.64** tu ndiyo ilikuwa imepokelewa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuwa fedha zinachoidhinishwa na Bunge zitolewe tena kwa wakati kwa lengo la kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

### **2.3.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ua Ofisi ya makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi.

#### **a) Utekelezaji wa Mpango na Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2017/2018**

##### **i) Makusanyo ya Mapatato**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira hufanya Makusanyo kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira - *NEMC*. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Baraza lilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi **15,683,161,500.00** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 8 Machi, 2018 Baraza lilikuwa limekusanya Shilingi **6,700,911,516.00** tu sawa na asilimia **42.7** ya makadirio yake, makusanyo haya yaliashiria ugumu wa kufikia lengo. Kamati inaendelea kuisisitiza kuwa lengo la maduhuli



linapaswa kupangwa kwa umakini mkubwa na kuzingatizingatia hali halisi.

**ii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha **2017/2018** Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira iliidhinishwa jumla ya Shilingi **9,634,020,437.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,845,568,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (mishahara na matumizi mengineyo ambayo ilijumuisha na ruzuku ya mishahara kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira) na Shilingi **5,788,452,437.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kati ya Shilingi **9,634,020,437.00**, zilizokuwa zimeidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira ni Shilingi **4,369,633,141.30** tu ndizo zilikuwa zimetolewa hadi kufikia 8 Machi, 2018. Kiasi hiki ni sawa na asilimia **45.3** ya fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hairidhishwi kabisa na mwenendo wa upatikaji wa fedha kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, Idara ya Mazingira. Utoaji huu wa fedha unakwamisha utendaji wa Ofisi hii muhimu katika uratibu wa masuala ya Mazingira. (kati ya Shilingi **3,845,568,000.00** zilizoidhinishwa kwa ajili matumizi ya kawaida ni Shilingi **1,875,032,651.30** tu ndizo zilizokuwa zimetolewa sawa na asilimia **48.4** ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida)

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/2018 (8 Machi, 2018) fedha za Miradi ya maendeleo, kati ya Shilingi **5,788,452,437.00** zilizotengwa ni Shilingi **2,494,600,490.00** tu ndizo zilizopokelewa ambazo pia ni fedha za nje na hakuna fedha za ndani zilizoidhinishwa Bunge zilizokuwa zimetolewa.

**Mheshimiwa Spika**, ikitokea wahisani wakaamua kusitisha ufadhili wao kwa miradi ya uhifadhi wa mazingira nchi itakuwa katika hali mbaya. Kamati inaishauri Serikali kulipa uzito suala la Uhifadhi wa Mazingira kwa kuongeza Bajeti ya Uhifadhi wa Mazingira na kuhakikisha fedha zinazoidhinishwa na Bunge zinatolewa tena kwa wakati.

**b) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**i) Makisio ya Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi Mazingira (**NEMC**) imepanga kukusanya shilingi **18,877,446,995.00** kutokana vyanzo vyake vya ndani. Makisio ya mwaka wa fedha **2018/2019** ambayo ni zaidi kwa asimia **20.4** ikilinganishwa na Shilingi **15,683,161,500.00** mwaka **2017/2018** ambazo hazitafikiwa, hivyo makadirio haya hayana uhalisia.

**ii) Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Idara ya Mazingira katika mwaka wa fedha **2018/2019** iliomba kuidhinishwa Shilingi **8,118,494,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni pungufu kwa asilimia **15.7** ikilinganishwa na Shilingi **9,634,020,437.00** kwa bajeti ya mwaka 2017/2018. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,524,540,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **4,593,954,000.00** ni matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Raisi kwa ujumla wake na kubaini kuwa mahitaji ya bajeti ya usimamizi na hifadhi ya mazingira ni makubwa kuliko kiasi kilichotengwa. Kamati

hairidhishwi na ukomo wa Bajeti ya Mazingira hivyo ni maoni ya Kamati kwa Serikali iangalie upya ukomo wa bajeti ya Ofisi hii muhimu.

## **2.4 TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Machi 2018 hadi Januari, 2019, Wajumbe walipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira taarifa hizo ni kama zifuatavyo:-

- a) **Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Maudhui ya Mwongozo wa Mageuzi ya Udhibiti ili kurahisisha Mazingira ya kufanya Biashara nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*)**

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*) ni matokeo ya malalamiko ya muda mrefu ya wawekezaji wenye viwanda na wafanyabisahara juu ya mazingira mabovu/magumu ya kufanyia biashara nchini. Andiko hili limetoa mapendekezo ya maboresho kwenye mazingira ya bisahara hususani mfumo wa udhibiti wa biashara na kuondoa mgongano baina ya mamlaka hizo, pia limeweka utaratibu wa kutekeleza sheria na sera mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, maeneo mahususi yaliyoguswa katika mpango huu ambayo yamekuwa yakilalamikiwa kwa muda mrefu ni pamoja na gharama kubwa za kuanzisha na kuendeleza biashara zinazotokana na wingi wa tozo; wingi wa mamlaka za Udhibiti ambazo majukumu yake yanaingiliana; na migongano ya sheria, kanuni na taratibu katika mamlaka mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** mazingira magumu ya kufanyia biashara yamekuwa yakiathiri ufanisi kwenye biashara na mwisho wa siku kupunguza utayari/ari kwa wawekezaji. Sambamba na hilo yamekuwa yakishawishi uvunjaji wa sheria na taratibu na kuleta vitendo vya rushwa na ufisadi kwa baadhi ya watendaji na wafanyabiashara wasio waaminifu.

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu inajielekeza katika kujenga Uchumi wa kati kupitia Ujenzi wa Viwanda ifikapo 2025 lakini mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu. Ugumu wa Mazingira ya kufanyia biashara umepelekea biashara nyingi kufungwa, hali hii inaashiria hata bidhaa zitakazoenda kuzalishwa katika viwanda tunavyoendelea kuvianzisha zitakosa soko na mwisho wa siku viwanda hivyo vitafungwa.

**Mheshimiwa Spika,** tumendelea kushuhudia nchi yetu ikizidi kushuka na kushika nafasi ya chini katika orodha ya nchi zilizokuwa na urahisi wa kufanya biashara (easy of doing business) kutoka nafasi ya 132 mwaka 2016 hadi nchi ya 144 mwaka 2019. Hali hii si nzuri na jitihada za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kujinusuru na uporomokaji huo.

**Mheshimiwa Spika,** matumaini ya Kamati pamoja na Wadau wote wa Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji yapo katika Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*). Kamati inaiomba Serikali kukamilisha mpango kazi wa utekelezaji mpango huu na utekelezaji wake uanze haraka iwezekanavyo. Sambamba na hilo Mpango huu uwe *flexible* kufanyiwa maboresho kadiri changamoto zinavyoendelea kujitokeza katika mazingira ya kufanyia biashara.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na mpango huu wa Serikali, pia tunatakiwa kutambua kuwa mazingira ya biashara yanajumuisha pia nchi za jirani, hivyo basi ili kuviwezesha viwanda na wafanyabishara wetu kushindana katika soko ni vyema wakati wa kupanga kodi/tozo na kutunga

sheria na kanuni mbalimbali zinazosimamia biashara tuzingatie nchi jirani wanafanya nini/vipi. Hatua hii itatatua changamoto ya sisi kuwa soko la biadhaa za wenzetu lakini pia itaziwezesha bidhaa zetu kushindana katika soko la ndani na nje ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na mipango mizuri ambayo hutuaminisha kuwa italetwa mabadiliko katika mazingira ya kufanya biashara ikiwepo Mpango wa kuboresha Mazingira ya Uwekezaji (*Business Environment Strengthening for Tanzania - BEST 2000*) na Programu ya kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (*Roadmap for Improving Investment Climate, 2009*) lakini ufuatiliaji wake umekuwa mgumu kutokana na kutokuwa na muda maalumu wa utekelezaji wake (time frame). Kamati inaishauri Serikali ipange muda maalumu (time frame) ya utekelezaji wa *Blueprint* kwa lengo la kuweza kupima ufanisi wake na kuainisha changamoto ambazo zimetatuliwa baada ya kipindi hicho kupita;

**b) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Shughuli zinazofanywa na Mamlaka ya EPZ pamoja na jitihada za Serikali katika kuhamasisha wazawa kuwekeza katika maeneo ya EPZ.**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya EPZ ni mamlaka ya Serikali iliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge (EPZ.Act, 2006) pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2008 na 2012 kwa lengo la kuandaa mazingira ya sekta ya Viwanda ambayo yataiwezesha Tanzania kuzalisha bidhaa ambazo zitaweza kushindana katika soko la kimataifa. Mamlaka ya EPZ imepewa jukumu la kusimamizi na kutekeleza Sheria na program za *Export Processing Zone (EPZ)* na *Special Economic Zone SEZ*.

**Mheshimiwa Spika,** EPZ ni maeneo maalumu ya uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya soko la nje, na ilianzishwa kwa madhumuni ya kujenga na kukuza Sekta ya Viwanda, kukuza mauzo ya nje, kuongeza ajira, kukuza

teknolojia, kuunganisha bidhaa zetu na masoko ya kimataifa na kuongeza thamani malighafi za ndani. SEZ ni mkakati wa kutekeleza 'Mini Tiger Plan 2020' na inalenga kuhamasisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini, SEZ ilianzishwa kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kukuza ushindani, kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuongeza pato na fedha za kigeni.

**Mheshimiwa Spika,** jukumu mahsusi la Mamlaka ya EPZ ni kuainisha, kutwaa, kuendeleza na kusimamia Kanda maalumu za Kiuchumi. Baada ya kutwa maeneo maalumu ya kiuchumia, huyaendeleza kwa njia tatu ambazo ni Mamlaka ya EPZ kumiliki maeneo kwa niaba ya Serikali, kuhaulisha au kukodisha maeneo kwa wawekezaji na EPZA kwa kushirikiana na Sekta Binafsi kuyaendeleza maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** viwanda vilivyopo ndani ya EPZ na SEZ vinapata fursa za:-kusamehewa kodi ya mapato ya makampuni (*Corporate tax*) kwa miaka 10 ya mwanzo; msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani - *VAT* na ushuru wa forodha kwa malighafi, vifaa, mashine na vifaa vya ujenzi vinavyonunuliwa hapa ndani ama kuagizwa kutoka nje; Msamaha wa kodi na ushuru unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa miaka 10 ya mwanzo; na faida nyingine za kiutaratibu kama vile kuwepo na huduma za TRA karibu, urahisi wa upatikanaji wa vibali vya kazi kwa watumishi watano wenye asili ya nje na kupata huduma zote muhimu chini ya mwamvuli wa EPZA.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na manuafaa na umuhimu mkubwa wa Mamlaka ya EPZ wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa rasilimali fedha kulinganisha na mahitaji halisi ya mamlaka jambo linalopelekea kukwamisha uendeshaji wa program za EPZ na SEZ; Ushirikiano hafifu kati ya Mamlaka ya EPZ na Taasisi/idara nyingine za Serikali katika kukamilisha baadhi ya shughuli mbalimbali za mamlaka; na Mamlaka ya EPZ msimamizi mkuu wa utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na kimkakati katika maeneo maalumu ya uwekezaji lakini inakabiliwa na changamoto

wa upungufu wa wataalamu wa fani muhimu jambo linalokwamisha ushiriki wao katika utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mhesimiwa Spika,** Kamati ilichambua taarifa ya Mamlaka ya EPZ na kubaini kuwa Sheria ya Mamlaka ya EPZ inaweza kuwa kikwazo. Sheria hii inamtaka Muwekezaji kuuza asilimaia **80** ya bidhaa anazozalisha nje ya nchi na asilimia **20** tu kuuzwa ndani, Sheria hii inaweza kuwa kikwazo kwa wawekezaji kwa sababu moja ya vivutio vya wawekezaji kutaka kuja Tanzania ni kupata soko pia. Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kubadilisha sheria hii na kuongeza walau asilimia chache za kuuza ndani hatua hii itawavutia wawekezaji wengi sababu soko lao litaongezeka;

**Mhesimiwa Spika,** aidha, Mamlaka ya EPZ imepewa jukumu la kutwaa maeneo, kuyalipia fidia na kuyaendeleza kimiundombinu kuhakikisha yanakuwa tayari kwa ajili ya uwekezaji, lakini upatikanaji wa fedha za maendelo kwa Mamlaka ya EPZ si wa kuridhisha (mfano katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilipokea asilimia 3 tu) jambo linalopelekea kukwamisha utekelezaji wa mamlaka hii. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe fedha zilizotengwa kwa ajili ya kazi hii zinapatikana tena kwa wakati ili kufanikisha jukumu hili kubwa;

**Mheshimiwa Spika,** kuna baadhi ya Maeneo yaliyotwaliwa na Mamlaka ya EPZ lakini mpaka sasa hayajalipwa fidia jambo linalowakwamisha wenye maeneo yao kujiendeleza katika maeneo mengine. Kamati inaishauri Mamlaka kutwaa maeneo machache ambayo itakuwa na uwezo wa kulipa fidia kwa wakati; Sambamba na hili Mamlaka ya EPZ ising'ang'anie kutwaa maeneo ya mjini ambayo yamegubikwa na migogoro, ijaribu kutwaa maeneo ya nje ya miji na kuyaendeleza kimiundombinu na kuyawekea vivutio ambavyo vitawavuta wawekezaji kwenda kuwekeza.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya Miradi chini ya Mamlaka ya EPZ utekelezaji wake umechukua muda mrefu sana, mfano Mradi wa Kurasini Logistic Centre unatekelezwa kwa takribani miaka Kumi (10) sasa na

Serikali imekwishawekeza fedha nyingi shilingi 191 (ambazo zimeshalipwa kama fidia), lakini bado hayajaanza kuwekezwa hivyo fedha zilizowekwa pale ni kama zimetelekezwa tu. Kamati inaishauri Serikali kuja na mpango wa haraka wa kuutekeleza mradi huu ili Taifa liweze kunufaika;

**Mhesimiwa Spika**, kuna baadhi ya wawekezaji chini ya mradi wa EPZ na SEZ wamekabidhiwa maeneo na wana nia ya kuyaendeleza lakini wamekuwa wakikumbana na mikwamo kutoka kwa mamlaka nyingine za Serikali na hivyo kupelekea kuchelewa kuyaendeleza. Kamati inaishauri Mamlaka ya EPZ kuweka utaratibu wa kuwatembelea wawekezaji mara kwa mara kwa lengo la kuwasikiliza changamoto zao na kuwasidia kuzitatua. Hatua hii itawavutia wawekezaji wengi kuwekeza nchini kwa kuona kuwa Serikali inawajali.

c) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Uendeshaji wa Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC);**

**Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) ilianzishwa mwaka 1968 chini ya Sheria ya Makampuni (*Companies Ordinance 212*) ikiwa ni ubia kati ya Serikali ya Tanzania chini ya NDC na Kampuni ya Kijerumani ya *Messrs Klockner INA* na kupewa jukumu ya kuendesha kiwanda cha kutengeneza mbole kilichokuwa Mkoani Tanga.

**Mheshimiwa Spika**, kiwanda kilianza kazi mwaka 1972 na kufanya kazi mpaka mwaka 1991 ambapo kilipata hitilafu na kusimama uzalishaji. Baada ya hitilafu hiyo Kampuni ya kijerumani ilijitoa na kukabidhi hisa zake kwa Serikali hivyo kuifanya Serikali kuwa mmilikiwa wa kiwanda kwa asilimia mia.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hitilafu ya mwaka 1991 TFC haikufanya kazi ya uzalishaji hadi kilipofungwa rasmi mwaka 1996 kupitia waraka wa Baraza la Mawaziri Namba 6 ambao ulieleza sababu ya kufungwa ni kutokana na kiwanda hicho kuwa katika eneo la makazi ya watu. Waraka



ulielekeza kuwa kiwanda kifungwe na mali zote za kiwanda ziuzwe. Pia ulielekeza kuwa kitengo cha biashara kibaki na kitafanya kazi ya kuagiza na kusambaza mbole.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kupitia taarifa ya TFC kamati ilibaini kuwa TFC inajijendesha kibiashara lakini kwa miaka mitatu mfululizo ilikuwa ikipata hasara. Kamati inaishauri Wizara kukifanyia tathimini na kubainisha kuwa kama ina umuhimu wa kuendelea kuwepo au kutokuwepo. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kujitoa katika uendeshaji wa TFC na kuibinafsisha kampuni hii, hatua ya kubinafsisha TFC itasaidia kupata uhakikika wa mbole, tutapata kodi na watanzania watapata ajira.

**Mheshimiwa Spika,** sheria, sera na miongozo ya usimamiazi wa masuala ya mbolea nchini yameonekana kuwa na ukakasi katika utekelzaji wake, Kamati inaishauri Serikali kuzipitia upya na kubaini dosari zilizopo na kuzirekebisha kwa manufaa ya wakulima wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imechaguliwa kuwa *Food Basket* wa kutekeleza mpango wa Chakula wa *Food Security* wa Afrika Mashariki. Maboresho ya sheria, sera na miongozo ya usimamizi wa mbolea itasaidia wakulima kuwa na uhakika wa mbolea na hatimaye tutapata mazao mengi na yenye ubora ili kukidhi mahitaji ya mpango huu;

**Mheshimiwa Spika,** utendaji wake TFC unahusiana moja kwa moja na shughuli za kilimo, kwa kulitambua hilo Kamati yangu ilishauri Serikali kuihamishia TFC chini ya usimamizi wa Wizara yake mama ya Kilimo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kupokea ushauri huu na sasa TFC imehamishiwa Wizara ya Kilimo.

- d) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mkakati wa Serikali wa kuliwezesha Shirika la SIDO kuhakikisha linafikisha huduma zake kwa watanzania wengi zaidi;**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 28 ya mwaka 1973 kwa lengo la kujenga msingi mzuri wa kuanzisha viwanda vidogo. SIDO imepewa jukumu la kusimamia uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vidogo na biashara ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya SIDO ni kuishauri Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu maendeleo ya viwanda vidogo na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo nchini, kupanga na kuratibu shughuli zote za miradi ya viwanda vidogo nchini, kufanya utafiti wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vidogo, kutoa huduma na mafuzo ya kiufundi kwa viwanda vidogo nchini

**Mheshimiwa Spika,** tunahamasisha wazawa kushiriki katika shughuli za uzalishaji na kuna muitikio mzuri hususani wakinamama wamekuwa wakijishughulisha na shughuli mbalimbali za ujasiriamali ikiwemo kuongeza thamani mazao hususani usindikaji. SIDO ndio ina jukumu la kuwasaidia wajasiriamali hawa lakini inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti. Bajeti inayotengwa kwa ajili ya SIDO hailingani na mahitaji halisi, pamoja na udogo wa bajeti hiyo bado haipelekwi kwa wakati hivyo kukwamisha utekelezai wa majukumu ya SIDO. Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti ya Shirika hili lakini pia kiasi kinachotengwa na kuridhiwa na Bunge kipelekwe kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** wajasiriamali wetu wanaanza kuendelea kwa kuanza kutumia mashine na mitambo katika kufanya shughuli zao hususani za uongezaji thamani mazao, lakini Shirika linashindwa kutengeneza mashine zinazoendana na mahitaji ya soko. Hili linasababishwa na mitambo iliyopo katika karakana za SIDO ni ya zamani

sana na inatumia teknolojia ya zamani. Kamati inaishauri Serikali kupitia SIDO kushirikiana na Taasisi/wadau wengine kuingia Ubia (Joint Venture) na sekta binafsi ili kununua mitambo ya kisasa.

**Mhesimiwa Spika,** wajasiriamali wanaojishughulisha na usindikaji wanakumbana na changamoto ya vifungashio, wamekuwa wakitegemea kuagiza vifungashio kutoka nchi ya Kenya ambavyo vinakuwa ghali na upatikanaji wake sio wa uhakika. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea nguvu SIDO kwa kuipatia fedha na teknolojia stahiki ili iweze kuwekeza katika uzalishaji wa vifungashio kwa wajasiriamali wetu ili waweze kuvipata kwa urahisi na uhakika.

- e) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Uendeshaji wa Taasisi ya TBS na Mkakati wa Serikali katika kuhakikisha TBS inafikisha huduma zake kwa watanzania wengi Zaidi**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linaendeshwa na Sheria Na. 2 mwaka 2009 na limepewa jukumu la kukuza matumizi ya viwango na kuinua ubora wa bidaa na huduma nchini kwa lengo la kupanua na kuimarisha soko la ndani na nje ya nchi. Sambamba na hili shirika linasimamia shughuli za utayarishaji wa viwango, udhibiti na uthibiti wa ubora wa bidhaa kutoka sehemu mbalimbali za ndani na nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** hatua zinazoweza kuchukuliwa mara baada ya kubaini uwepo wa bidhaa hafifu sokoni zimebainishwa katika Sheria ya Shirika la Viwango Tanzania ambazo ni kuziondoa sokoni; kuweka utaratibu wa kiziharibu au kuzirudisha zilikotoka; kumtoza faini muuzaji/msambazaji; na kusitisha leseni au cheti cha ubora wa bidhaa cha mzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia uhakiki wa ubora wa bidhaa tutaweza kuisaidia nchi yetu kutimiza azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda kwani bidhaa zetu zitakuwa na ubora wa kimataifa na hivyo kupata soko ndani na nje ya nchi. Katika harakati za kujenga Tanzania ya Viwanda tunategemea uwekezaji mpya unakuja kufanyika lakini TBS bado haina uwezo wa kutoa viwango vya bidhaa hizo (mfano Viwanda vya magari). Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha TBS kupata mafunzo stahili ambayo yataliwezesha Shirika kuwa na uwezo wa kukagua uwekezaji mpya unaoendelea kufanyika;

**Mheshimiwa Spika,** TBS imepewa jukumu la kuinua ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini lakini tumeshuhudia wajasiriamali wengi wadogo wamekuwa wakipata changamoto za masoko ya bidhaa zao kwa sababu ya kukosa viwango (hali hii inachangiwa na kukosa elimu viwango). Kamati inaishauri Serikali kuwasadia wazalishaji wa ndani kwa kuwapatia elimu ya viwango na kuhakikisha wanazalisha bidhaa zinazoweza kushindana kwa ubora katika soko;

**Mheshimiwa Spika,** Watanzania wengi wamekuwa wakitumia bidhaa zisizokidhi viwango, jambo hili hutokana na kuendelea kuwepo kwa bidhaa hizo katika soko lakini pia kutokana na unafuu wa bei za bidhaa. Kamati inaishauri Shirika kuongeze kasi katika kutoa elimu juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa zisizokidhi viwango vya ubora. Hatua hii itasaidia kuepuka madhara lakini pia itachochea ushindani wa haki.

**Mheshimiwa Spika,** TBS imekuwa ikitumia mawakala wa Pre-shipment Verification of Conformity (PVOC) kufanya ukaguzi wa bidhaa kabla hazijaingizwa nchini. Taarifa zilizopo ni kwamba mawakala wa PVOC wamekuwa na tabia ya kutokagua mizigo, wanachokifanya wanaangalia cheti cha TBS cha kiwanda kilipotoka bidhaa na kutoa cheti kama imeukagua na kuthibitisha mzigo. Kamati inatambua nia njema ya Serikali kuamua kutumia mfumo wa PVOC kwa lengo la kupunguza msongamano

bandarini lakini kutokana na urasimu unaoendelea katika mfumo huu, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya namna ya kuachana na PVOC na kuamua kuendelea na utaratibu wa bidhaa kukaguliwa hapa nchini tu.

**Mheshimiwa Spika,** TBS haina kiwango kimoja cha gharama kwa huduma ya aina moja jambo ambalo linanatoa picha ya urasimu na kupelekea baadhi ya wafanyabiashara kuamua kutumia njia za panya kwa lengo la kuwakwepa TBS. Matokeo ya ukwepaji huu ni kukosa kodi lakini pia kuendelea kuwa na bidhaa zisizokidhi viwango sokoni. Kamati inaishauri Serikali *kuestablish* gharama za huduma zao TBS ambayo itakuwa sawa kwa huduma za aina moja.

f) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mpango wa Serikali katika Kufungamanisha shughuli za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi na Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kiasi kikubwa nafasi za ajira Viwandani zimechukuliwa na kutekelezwa na mitambo ya roboti (*robotic machine*), kwa kuzingatia hilo Serikali inatakiwa kuchukua jitihada za makusudi za kufungamanisha shughuli za kilimo, ufugaji uvuvi na ujenzi wa Viwanda kwa lengo la kuongeza ajira ukizingatia kuwa shughuli hizi ndio kimbilio na tegemeo la Watanzania walio wengi.

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) umeelezea nia ya kuanzisha viwanda vitakavyo ajiri watu wengi, kuanzisha viwanda vinavyotumia malighafi nyingi zinazopatikana nchini na kutoa ajira, kuanzisha viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazotumika kwa wingi nchini. Utekelezaji wa mpango huu unapaswa kwende sambamba na kufungamanisha shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji na ujenzi wa viwanda nchini kwa lengo la kuimarisha

sekta hizi sambamba na kuimarisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi kutoka kwa sekta hizi.

**Mheshimiwa Spika,** tumeshuhudia mazao yetu mbalimbali yakikumbana na changamoto ya kupata masoko jambo lililopelekea mpaka kushuka thamani kwa mazao. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi za kuhamasisha ujenzi wa viwanda ambavyo vitaenda kuchakata mazao yetu hususani mazao ya kipaumbele. Sambamba na kuhamasisha ujenzi wa viwanda hivyo, tuwahamasishe wakulima wetu kufanya kilimo cha kisasa kwa lengo la kupata mazao mengi na yenye ubora unaotakiwa.

**Mheshimiwa Spika,** mazao yetu yamekumbwa na changamoto ya bei na masoko mfano mazao ya mahindi, mihogo, korosho, mtama, pamba, kahawa chai, pareto na tumbaku. Kwa mazao ya mahindi, mabibo na mihogo yanaweza kutumika kuzalisha nipa, ambayo inatumika katika kuzalisha pombe kali. Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali vya kutumia mazao ya mahindi, mabibo na mihogo kuzalisha nipa kwa lengo la kuwasaidia wakulima wa mazao haya kupata soko la bidhaa zao lakini pia kuongeza ajira kupitia kilimo cha mazo hayo na wenyeviwanda kupata malighafi (nipa) kiurahisi na kwa gharama nafuu na kusaidia kupunguza mahitaji ya fedha za kigeni;

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania imebarikiwa kuwa nchi ya pili Barani Afrika kwa wingi wa mifugo hivyo kutuweka kwenye nafasi ya kuwa na malighafi ya ngozi ya kutosha. Pia, mahitaji ya bidhaa za ngozi nchini ni makubwa (viatu, mikoba, mabegi, makoti na mikanda). Uwepo wa malighafi na mahitaji ya bidhaa za ngozi inatuweka katika nafasi nzuri ya kunufaika na hatua ya kufungamanisha viwanda na shughuli za ufugaji, Kamati inaishauri Serikali kuhamasishwa uwekezaji katika viwanda vya bidhaa za ngozi.

**Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya ngozi katika soko la Dunia yamekuwa makubwa kwa kuwa kuna baadhi ya nchi huitumia kama chakula, Kamati

inatambua nia njema ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuvilinda viwanda vya ndani kwa kuweka *export levy* ya 80% kwa Dolla 37 kwa tani moja. Kamati inaishauri Serikali kutambua mahitaji ya viwanda vya ndani kisha kuruhusi kiasi kilichobaki kuuzwa nje ya nchi, sambamba na hilo Serikali iangalie namna ya kuishawishi Jumuiya kupunguza *export levy* kwa lengo la kutoa fursa kwa wafugaji wetu kuuza ngozi ambazo kwa sasa zimekuwa zikitupwa na kuchafua mazingira (Tanzania ndio wahanga wakubwa wa kodi hiyo kwa kuwa sisi ndio wazalishaji wa kubwa wa ngozi katika Jumuiya ya EAC).

**Mheshimiwa Spika,** zao la alizeti limeonekana kuwa zao mkombozi kwa wakazi wa ukanda wa Singida na Dodoma. Pamoja na kuwa na viwanda vidogo vidogo vingi katika ukanda huo bado tumeshuhudia wajasiriamali wadogo wadogo wakijipatia riziki kupitia kilimo cha alizeti na shughuli za kukamua mafuta na kuyauza barabarani. Wajasiriamali hawa hawana eneo maalumu la kufanyia shughuli zao za ukamuaji mafuta pia wanatumia teknolojia duni hivyo kuyafanya mafuta yao kukosa ubora unao stahili. Kamati inaishauri Serikali kuangalie namna nzuri ya kuwaunganisha wazalishaji wadogo wa mafuta ya alizeti kwa kuwapatia eneo maalumu la uzalishaji na uuzaji wa bidhaa zao. Sambamba na hilo iwawezeshe kupata mashine ya kuchuja mafuta kwa lengo la kuongeza ubora na thamani ya mafuta ya alizeti, hatua hii itarahisisha pia Serikali kupata mapato stahiki;

**Mheshimiwa Spika,** kilimo ni kimbilio na tegemeo la Watanzania walio wengi hivyo juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kuimarisha shughuli za kilimo nchini. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango wa kuwahamasisha na kuwasaidia wakulima wetu kupata na kutumia mbegu bora kwa lengo la kupata mazao mengi na yenye ubora unaokidhi soko.

- g) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) na Mipango ya CAMARTEC katika kutengeneza zana za kilimo zinazoendana na mahitaji ya wakulima vijijini;**

**Mheshimiwa Spika,** Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) ni muunganiko wa Taasisi ya Majaribio ya zana za kilimo- (TAMTU) na Mradi wa Uendeshaji wa Taknolojia Arusha – AATP ambao ulilenga kuboresha maisha ya wananchi kupitia uendeshaji na uhaulishaji wa teknolojia za zana za kilimo, nishati, maji safi na taka, vifaa vya ujenzi na majengo vijijini.

**Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC inatazamiwa kutoa teknolojia zenye kuleta maendeleo ya kilimo kwa jamii za vijijini nchini. Katika kutekeleza hili CAMARTEC inatekeleza majukumu ya kufanya utafiti katika zana za kilimo na teknolojia zinazofaa kutumika vijijini kwa lengo la kuleta maendeleo ya kilimo kwa wananchi waishio vijijini; kutengeneza sampuli kifani (*prototype*) zilizothibitishwa na kisha kuzitathimini ili kubaini ubora na uwezo wa kutumika katika mazingira ya Tanzania; kurekebisha (*adapt*) teknolojia za kigeni za zana za kilimo ili ziweze kuendana na mazingira ya Tanzania; kuendesha mafunzo ya muda mfupi ya nadharia na vitendo yanayohusu zana za kilimo na teknolojia; kutoa huduma za ushauri elekezi juu ya ubunifu, majaribio ya kiufundi kuhusu zana za kilimo; na kuwa muwakilishi wa Taifa na katika majukumu ya kituo katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** CAMARTEC imefanikiwa kubuni na kuunda trekta aina ya *CAMARTEC Fastrucktor-CFT* sambamba na kulifanyia majaribio na kufanya ufuatiliaji wa utendaji wake; kubuni na kuunda kipandio (*planter*) cha mbegu za pamba; kubuni na kuunda mashine za kipura mazao ya kilimo (mashine ya kupura na kupeta mtama, uwele, maharage, alizeti, dengu, ngano na mpunga); mashine ya kukata na kufunga majani ya



malisho ya mifugo. Aidha, Kituo kimekuwa na miradi mbalimbali ya ujenzi wa mitambo ya nishati mbadala (biogesi) katika taasisi na kaya mbalimbali. Pia kituo kinajihusisha na tafiti za maeneo ya nishati ambapo kwa sasa inashirikiana na Tanzania Breweries Ltd (TBL) kafanya tafiti katika chachu ya bia iliyotumika kwa nia ya kuzalisha biogesi.

**Mheshimiwa Spika,** kilimo ni uti wa mgongo wa watanzania wengi uwepo wa taasisi hii utawasaidia wakulima wetu kwa kuwarahisishia kazi kuanzia kwenye hatua ya kulima, kupanda na kuvuna. Kamati inashauri Wizara kukitengea kituo bajeti ya kutosha na fedha zipelekwe kwa wakati ili kiweze kufikisha huduma zake kwa wahitaji wengi zaidi hatimaye kuwasaidia wakulima wetu kuzalisha kwa kiwango kikubwa tena mazao bora yatakayokidhi mahitaji ya soko;

**Mheshimiwa Spika,** kituo kinatumia teknolojia duni sana jambo linalopelekea kuzalisha mashine zinazohusisha nguvu nyingi katika kuzitumia, Kamati inaishauri Serikali kukiwezesha kituo hiki kupata teknolojia mpya ambayo itawawezesha kuzalisha mashine ambazo zipo *softicated* kidogo kwa lengo la kuwarahisishia wakulima wetu kazi;

**Mheshimiwa Spika,** kilimo ni shughuli inayotegemewa na kufanywa na watanzania walio wengi hususani wa hali ya chini, Kamati inaishauri Wizara kutenga bajeti ya kituo ambayo itawawezesha kutosheleza gharama za uzalishaji na kukiwezesha kituo kuuza zana zao kwa gharama nafuu na kuwanufaisha watu wa hali zote;

- h) **Utendaji wa Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO); na Mipango ya TEMDO katika kuwezesha upatikanaji wa vifaa/zana zinazoendana na mnyororo wa kuongeza thamani kwenye mazao mbalimbali.**

**Mheshimiwa Spika,** mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka mitano (1975/76 – 1979/80) ulitilia mkazo uanzishaji wa viwanda vua msingi. Mpango huu ulipelekea kuundwa kwa Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) kwa lengo la kulijengea taifa uwezo katika kubuni, kusanifu na kuunda mashine na mitambo kwa ajili ya sekta mbalimbali za uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya TEMDO ni pamoja na; kutafiti, kubuni na kuunda mitambo, mashine teknolojia pamoja na vifaa mbalimbali na kuhamasisha utengenezaji vilivyobuniwa kibiashara; kutoa huduma za kihandisi kwenye viwanda vikubwa, vya kati na vidogo kwa lengo la kuongeza ufanisi, matumizi bora ya rasilimali, ubora wa bidhaa na uwezo wa ushindani; na kutoa mafunzo kwa wahandisi na mafundi mchundo viwandani ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Shirika linakabiliwa na changamoto kubwa ya uhaba wa fedha jambo ambalo linapelekea Shirika kushindwa kujitangaza na kusambaza mitambo na mashine zilizozalishwa na shirika kwa kiwango cha kuwafikia walengwa. Pia, Shirika halina mazingira ya mazuri ya kufanyia kazi pamoja na vitenda kazi vya kutosha katika kuendeleza shughuli za ubunifu na undelezaji wa teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuwa, TEMDO imejipanga kubuni na kutengeneza zana kulingana na mahitaji ya tathimini iliyofanywa na kubaini zana zinazohitajika kwa sasa katika mfumo mzima wa uongezaji thamani mazao yetu kwa lengo la kuwarahisishia wakulima wetu katika zoezi zima la kulima, kupanda na kuvuna;

**Mheshimiwa Spika**, ufinyu wa bajeti imekuwa tatizo sugu kwa taasisi zetu za utafiti (CAMARTEC, TEMDO, SIDO, TIRDO) jambo linalowakwamisha kujitangaza na kufikisha huduma zao kwa watu wengi. Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi hizi ziweze kuungana (*team up*) na kuandaa matangazo na kufanya semina kwa pamoja. Hatua hii itawawezesha kujitangaza zaidi kwa kutumia rasilimali ndogo waliyonayo ukizingatia kuwa taasisi hizi zinafanya kazi zinazoendana haitakuwa ngumu. Aidha, Kamati imevielekeza vituo hivi kuwasiliana na Halmashauri zote nchini kupitia kitengo cha Biashara katika kutoa elimu ya huduma wanazozitoa;

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa mashirika mengine ya utafiti chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara TEMDO pia inatumia teknolojia duni/ya zamani sana jambo linalosababisha kuzalisha mashine ngumu (zakizamani sana) kulingana na mahitaji ya soko la sasa. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha TEMDO kupata teknolojia ya kisasa ili iweze kuzalisha mashine *softicated* kwa lengo la kuwarahisishia kazi watumiaji.

i) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC); na Mpango wa Serikali katika kuvutia uwekezaji kwenye Sekta zinazofungamanishwa na Ujenzi wa Viwanda.**

ii) **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Uwekezaji Tanzania - *TIC* kiliundwa Septemba, 1997 baada ya kufutwa kwa iliyokuwa Taasisi ya Kuhamasisha Uwekezaji - *IPC* ya mwaka 1990. *TIC* inaendeshwa na Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997, na ina jukumu kuu la kuratibu, kuhimiza, kuhamasisha, kuwezesha na kuishauri Serikali kuhusu Sera sahihi na mambo mengine yanayohusu uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya *TIC* yameainishwa katika kifungu cha 5 cha sheria ya Uwekezaji ambayo ni pamoja na Kubuni mbinu za kujenga mazingira bora ya uwekezaji nchini kwa lengo la kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi; kusaidia wawekezaji kupata vibali mbalimbali na hati

za kisheria; kuandaa na kusambaza taarifa sahihi kuhusu fursa za uwekezaji na upatikanaji wa mitaji na wabia; kuwahamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika sekta muhimu zitakazokuza uchumi kwa haraka; na kushirikiana na Serikali kutafuta maeneo ya uwekezaji na kuyatayarisha kwa muwekezaji kuja na kuanza uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa kuhusu mpango wa Serikali katika kuvutia uwekezaji kwenye sekta zinazofungamanishwa na ujenzi wa Viwanda, mpango huo umejielekeza katika kutekeleza Mpango wa Pili wa Maendeleo ambao unaelekeza kuendeleza na kuhamasisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi kama vile nguo, ngozi, mafuta ya kula, katani, sukari, matunda; kuimarisha programu za uhamasishaji na uwekezaji kupitia taasisi zinazosimia uwekezaji (TIC, EPZA na Tantrade); kuimarisha upatikanaji wa masoko ya ndani na nje ya nchi; na kusimamia upatikanaji wa mitaji.

**Mheshimiwa Spika,** TIC inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Uwekezaji, mabadiliko ya kila mwaka ya Sheria ya Fedha yamekuwa yakiathiri utekelezaji wa Sheria ya Uwekezaji hususani katika kipengele vivutio vya uwekezaji na kodi. Kamati inashauri Wizara ya Fedha wakati wa kufanya Mapitio na Mabadiliko katika Sheria ya Fedha ikae pamoja na Kituo cha Uwekezaji Tanzania-TIC na kupitia Sheria ya Uwekezaji kwa lengo la kupata makubaliano yenye faida kwa pande zote mbili;

**Mheshimiwa Spika,** Sera na Sheria za uwekezaji hazikidhi matakwa ya sasa ya kuvutia na kuhudumia wawekezaji, kuna badhi ya maeneo yanahitaji maboresho. Maeneo yanayohitaji maboresho ni pamoja na kuizuia Sheria ya Uwekezaji kuathiriwa na mabadiliko ya sheria nyingine ikiwepo Sheria ya Fedha, Vivutio vya uwekezaji kwa kuingizwa kwenye Sheria ya Uwekezaji badala ya Sheria ya Fedha na kuimarisha huduma za *One stop shop*.

**Mheshimiwa Spika,** upatikanaji wa ardhi kwa wawekezaji umekuwa na mlolongo mkubwa na hata pale inapopatikana imekuwa na migogoro

mingi kati ya wawekezaji na wakazi wa aneo husika, aidha mchakato wa kuhaulisha ardhi kutoka ardhi ya kijiji kwenda ardhi ya jumla unachukua muda mrefu sana kati ya miaka miwili hadi mitatu (kwa wawekezaji wa nje hata wa ndani) jambo linalopelekea wawekezaji walio wengi kushindwa kuvumilia kuendelea kusubiri. Kamati inashauri kuwa katika kutenga maeneo ya uwekezaji tuangalie maeneo ya nje ya miji ambayo hayamilikiwi na watu hivyo kukwepa suala la fidia na mivutano na wananchi. Pia, itolewe elimu kwa wananchi juu ya umuhimu na faida za uwekezaji hatua ambayo itapunguza migogoro kati yao kwa kuwaona wawekezaji ni wanyonyaji lakini pia itawawezesha kushiriki katika shughuli za uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli nyingi za uwekezaji zimekuwa zikifanyika katika maeneo ya mijini, jambo hili kwa kiasi kikuwa linasababishwa na kukosekana kwa huduma mbalimbali (maji, umeme, barabara n.k) katika maeneo ya nje ya miji. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna katika Sheria yake ya Uwekezaji kuweka *Modal* ambayo itawaruhusu Wawekezaji kuvuta Huduma hizo katika maeneo yao kisha gharama wanazotumiwa zifidiwe katika bili ya matumizi watakazofanya;

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na matamko mbalimbali kutoka kwa viongozi wa Mamlaka wa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo utekelezaji wake unaathiri hali ya Uwekezaji Nchini. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na TIC Kuandaa miongozo mbalimbali ambayo itawasimamia Viongozi hao katika kusimamia mambo ya Viwanda na uwekezaji;

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa Kituo cha Uwekezaji Tanzania- TIC kimehamishiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

- k) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani (WRRB); na Mpango wa Serikali katika kutatua changamoto za uendeshaji wa maghala.**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani (WRRB) ni Taasisi ya Serikali iliyoazishwa kwa Sheria ya Stakabadhi Ghala Na.10 ya mwaka 2005. Mfumo wa Stakabadhi Ghala ni aina ya biashara ambapo bidhaa zinahifadhiwa ndani ya ghala lenye leseni na mmiliki wa bidhaa anapewa stakabadhi inayoonyesha umiliki mahsusi, thamani, aina, idadi na ubora wa bidhaa iliyowekwa ghalani. Mfumo huu unalenga kurasimisha mfumo wa masoko kwa lengo la kutafuta mazao ya kilimo, lakini pia kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyokinzana na uzalishaji wenye tija.

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Taasisi hii ni kutoa leseni kwa waendesha ghala; kutoa leseni kwa wakaguzi wa ghala; kuendesha mfumo wa kisasa na makini wa Stakabadhi ghala; kutangaza mfumo wa Stakabadhi ghala; kuratibu shughuli za wadau wa mfumo wa stakabadhi ghala; kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa za mfumo wa Stakabadhi ghala kwa wadau; kushirikiana na vyombo vingine vya kitaifa na kimataifa vinavyofanya kazi kama za Bodi; na kuishauri na kuiwakilisha Serikali kwenye mikutano au makongamano yanayojadili mfumo wa Stakabadhi ghala;

**Mheshimiwa Spika,** watumiaji wa mfumo huu wananufaika na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwawezesha wamiliki wa stakabadhi ghala kuzitumia stakabadhi zao kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha; kuongeza ushiriki wa wafanyabishara wa bidhaa za mazao katika biashara za kimataifa; kuongeza upatikanaji wa sehemu za kuhifadhi mazo zilizo bora, kupunguza hasara za baada ya kuvuna na kuimarisha uhakika wa chakula; kuunganisha mfumo mdogo wa ugani na pembejeo; kupata taarifa za soko na mauzo za kuaminika kwa wadau.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu na faida zipatikanazo kwa kutumia Mfumo wa Stakabadhi Ghala, bado Bodi inakabiliwa na

changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na upungufu wa rasilimali fedha, watu na vitendea kazi hivyo kukwamisha bodi kufika kwenye maeneo mengi lakini pia kushindwa kuhudumia mazao mengi; uhaba wa maghala bora ya kuhifadhi mazao, maghala mengi yaliyopo yanamilikiwa na watu binafsi hivyo uhakika wa kumnufaisha mkulima kwanza inakuwa changamoto; uelewa mdogo juu ya mfumo wa stakabadhi ghala hali inayopelekea baadhi ya wadau walanguzi kuwapotosha wananchi kwa maslahi yao binafsi;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijulishwa mpango ya Serikali katika kutatua changamoto za uendeshaji ghala utahusisha kushirikiana na soko la bidhaa kutengeneza mfumo wa kielektronik wa stakabadhi ghala na soko la bidhaa; kushirikisha taasisi/wadau wa sekta ya umma katika kutoa elimu ya Mfuko wa Stakabadhi Ghala; katika kutatua changamoto ya upungufu wa rasilimali fedha Bodi imeandika maandiko mbalimbali na kuyatuma katika mashirika ya wafadhili kama Common Fund for Commodities na Agricultural Market Development Trust (AMDT);

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kuiwezesha Bodi hii muhimu kwa kuipatia rasilimali watu na fedha ili kuweza kuhudumkia mazao mengi zaidi na hatimaye kuongeza ajira kupitia kilimo kwa kuwa watakuwa na uhakika wa soko. Aidha, Kamati inaomba kuona uwezesaji wa Bodi hii unafanyika katika Bajeti ijayo ya Wizara yani Mwaka wa Fedha 2019/2020;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na huduma nyingine zitolewazo na Bodi, Kamati inaishauri Serikali kupitia Bodi hii isaidie kuwapatia wakulima wetu elimu ya huduma za kifedha, hatua hii itasaidia kuwaepusha kuchukuwa fedha (mikopo) kwa walanguzi na mwisho wa siku faida wanayoipata inaishia kulipa madeni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha Bodi ya Stakabadhi Ghala kwa lengo la kufanikisha kuunganisha Ujenzi wa Viwanda Nchini na Shughuli za Kilimo ambazo ndio shughuli kuu ya watanzania walio wengi. Tutumie Bodi kukusanya mazao ya wakulima na kuleta uhakika wa malighafi kwa viwanda vinavyotumia mazao ya kilimo. Suala hili liende sambamba na kujenga maghala mengi zaidi kwa lengo la kuhakikisha angalau asilimia kuwa ya mazao/wakulima wanaohitaji huduma hii ya Stakabadhi Ghalani wanaipata;

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Stakabadi Ghala inasimamia mazao ambao usimamizi wake upo chini ya Wizara ya Kilimo na kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara jukumu lao kubwa ni kutoa leseni tu kwa maghala na wawendesha maghala. Kamati inashauri usimamizi wa Bodi hii uhamishiwe kwa wizara mama ambayo ni Wizara ya Kilimo.

l) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utendaji wa Kiwanda cha URAFIKI;**

**Mheshimiwa Spika,** URAFIKI ni kiwanda cha ubia kati ya Serikali ya Tanzania (49%) na Serikali ya China kupitia kampuni ya *Chanzhou State Owned Textile Assets Operations Company Limited* (51%). Kiwanda kinazalisha nguo kuanzia hatua ya uchakataji wa pamba hadi kitambaa kilichotiwa rangi. Kiwanda hiki kilianza uzalishaji kama Shirika la uma miaka ya 1968 na uwezo wa uzalishaji ulikuwa mita milioni 33 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** katika miaka 22 ya Ubia (1996 hadi 2028) Kiwanda cha URAFIKI kimekuwa kikipata hasara, hasara ya kiwanda hiki inatokana na kuzalisha chini ya uwezo wa kiwanda ambao unatokana na kutumia teknolojia na mitambo ya zamani sana. Kamati inatambua uchakavu wa teknolojia ya miaka 1968 lakini inatambua pia lengo la kuingia Ubia lilikuwa ni kuongezaa nguvu katika kiwanda lakini pia kuleta teknolojia mpya.



**Mheshimiwa Spika,** aidha, kati ya miaka ya 1996 na 2008 kiwanda kimechukua mikopo ya jumla ya Yuan 217,150,000 kwa malengo tofauti tofauti ikiwemo la kuboresha Teknolojia ya kiwanda. Kamati haifahamu mkopo huo ulitumika kufanya nini kwa kuwa changamoto ya teknolojia duni ya kiwanda bado ipo mpaka leo.

**Mheshimiwa Spika,** tumeshuhudia bidhaa za kiwanda cha URAFIKI zikipendwa sana sokoni, lakini uzalishaji wa kiwanda hauendani na mahitaji ya soko hivyo kutoa mianya wafanyabishara wasio waaminifu kuingiza sokoni kopi ya bidhaa za URAFIKI jambo ambalo si haki. Kamati inaishauri Serikali kufanya upembuzi yakinifu kwa kiwanda na kubaini changamoto hasa ya kiwanda ni nini. Sambamba na hilo atafutwe muwekezaji mwingine mwenye nia njema ya kutaka kuwekeza katika kiwanda chetu.

**Mheshimiwa Spika,** asili ya shughuli katika viwanda vya nguo husababisha viwanda hivyo kuajiri watu wengi zaidi, mfano ni hiki kiwanda cha URAFIKI kilikuwa kimeajiri watu elfu mbili (2000). Kwa sasa ajira zipo chini ya mia nne (400), kufufuka kwa kiwanda hiki na kukiwezesha kuzalisha kwa uwezo wa kiwanda kutatoa ajira kwa watanzania. Kamati inashauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kiwanda huki kinafufualiwa.

**Mheshimiwa Spika,** nikweli kuwa kiwanda kilianza kufanya vibaya kabla ya kuingia ushirika na Nchi ya China lakini baada ya ushirika kiwanda kimefanya vibaya zaidi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia jambo hili kwa ukaribu zaidi, sambamba na hilo jitihada za makusudi zichukuliwe ili kuhakikisha kuwa tunaendelea kulitawala soko kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

m) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Mpango wa Serikali wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa; na Jitihada za Serikali katika kuviridisha Serikalini viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo wamiliki wake wameshindwa kuviendeleza.**

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira walipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Mpango wa Serikali wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa; na Jitihada zinazochukuliwa katika kuvirudisha Serikalini viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo wamiliki wake wameshindwa kuviendeleza. Uchambuzi wa Kamati ulibaini taarifa ile haikuwa na maelezo ya kujitosheleza hivyo inahitaji maboresho kwa lengo la kuongeze uelewa wa Wajumbe na kuwawezesha kuisahuri Serikali. Maeneo yaliyohitaji maboresho ni pamoja na;-

- i) Sababu zilizobainishwa kupelekea viwanda kutokufanya kazi hazina uhalisia kwani Viwanda vyote viliuzwa kwa kuzingatia Mpango wa kibiashara (*Business plan*) lakini pia wamiliki walipewa mikataba yenye masharti ya kuviendesha viwanda vile. Kamati inataka kujua kinachokwamisha Serikali kuwachukulia hatua wale wote waliokiuka Mikataba na masharti kwa kuwa mikataba tayari ilikwisha wafunga;
- ii) Kuna idadi ya Viwanda 156 vilivyobinafsishwa, Kamati inataka kujua ni Viwanda vingapi vinaweza kurudishwa/kufufuliwa na kuweza kufanya kazi na vingapi haviwezekani kufufuliwa ili vitoke katika idadi ya viwanda vilivyopo nchini; na nini Mpango wa Serikali wa kuyatumia maeneo ya viwanda vilivyo shindikanika kwa shughuli nyingine za maendeleo.
- iii) Kuna baadhi ya mikataba iliyotumika kubinafsisha Viwanda hivi haikuwa na kipengele kinachotoa nguvu ya kuvirudisha Serikalini. Kamati inahitaji kujua mikataba hii ilisainiwa vipi bila kuwa na kipengele hicho na hatua gani zinachukuliwa kutatua changamoto ya mikataba hii;

- iv) Kuna baadhi ya Viwanda vimetajwa kuwa chini ya uangalizi wa Serikali, hakuna maelezo ya namna Serikali inafanya uangalizi kwa kiwanda hivyo;
- v) Toka Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na Viwanda umefanyika ni takriban miaka 20 sasa, katika kipindi chote hicho kuna baadhi ya Viwanda havikuwahi kufanya kazi tarajiwa kabisa. Kamati inataka kujua ni hatua gani zimechukuliwa na Serikali dhidi ya wamiliki wa viwanda hivyo.
- vi) katika zoezi la kuhamasisha kufufua viwanda vilivyobinafsishwa, kuna baadhi ya wewekezaji wameitikia wito wa Serikali wa kufufua viwanda walivyobinafsishiwa, walivifufua na kufanikiwa kuviendeleza lakini ndani ya mwaka mmoja tu wamevifunga. Kamati inataka kujua ni hatua gani za zaidi zimeendelea kuchukuliwa na Serikali katika eneo hili.

**Mheshimiwa Spika**, katika viwanda vilivyobinafsishwa kuna viwanda kumi (10) vinafanya kazi vizuri ikiwepo kiwanda cha Sigara (TCC), kiwanda cha mabati cha ALAF, Kiwanda cha bia TBL n.k. Kamati inaishauri Serikali kuvienzi viwanda hivi vya kihistoria, sambamba na hilo tubainishe changamoto zinazovikabili viwanda hivi na kuzishughulikia kwa lengo la kuviondoa katika hatari ya kufungwa kama vyeenzake;

**Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, baada ya kuona kuna uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo** aliamua kuanzisha viwanda vya kuchakata mazao hayo kwa nia ya kuyaongezea thamani mazao lakini pia alilenga kuchochea ukuaji wa uchumi na kutoa ajira. Viwanda vile vya kihistoria vilipitia hatua tofauti tofauti na hatua ya mwisho ilikuwa ni kuvibinafsisha kwa lengo la kuviendeleza viwanda hivyo, kuongeza ajira na mapato ya Serikali kupitia kodi na kuiruhusu sekta binafsi kumiliki uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, jitihada za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa kwa lengo ka kutimizi madhumuni halisi ya ubinafsishaji.

- n) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa KAIZEN; Mpango wa Serikali katika kutumia falsafa ya KAIZEN; Namna Serikali inavyoishirikisha Sekta Binafsi (CTI, TPSF na TCCIA n.k) katika utekelezaji wa Mradi wa KAIZEN.**

**Mheshimiwa Spika,** KAIZEN ni neno lililotoholewa katika lugha ya kijapani linalomaanisha *Change for Better*, KAIZEN ni mfumo wa kuweka hali ya maelewano na ushirikiano miongoni mwa watumishi na uongozi katika kutumia mbinu bunifu kwa lengo la kuleta mabadiliko chanya katika kuimarisha ubora, uwajibikaji na tija endelevu kwenye kampuni au kiwandani katika mlolongo mzima wa uzalishaji ili kukidhi ushindani.

**Mheshimiwa Spika,** falsafa ya KAIZEN inalenga kuleta mabadiliko ya mtizamo wa watendaji wa viwanda ili kuongeza ufanisi, tija na ubora wa bidhaa. Zimeandaliwa programu mbalimbali za kufundishia chini ya KAIZEN ambapo mkufuzi kufikisha elimu kupitia programu hizo, mkufunzi pia huzungukia eneo la kiwanda na kubainisha changamoto za kiwanda kwa lengo wa kuwapatia huduma hiyo kulingana na mazingira halisi ya kiwanda chao. Tija ya utekelezaji wa falsafa hii huanza kuoneka mara baada ya mafunzo ambapo mabadiliko makubwa hupatikana kuanzia katika ari ya wafanyakazi, mahusiano ya wafanyakazi na waajiri na hata katika uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa utekelezaji wa falsafa hii umehusisha Sekta binafsi ambapo wanaanza kushirikishwa kuanzia kwenye Kamati ya Kitaifa ya kusimamia Mradi kama wajumbe wa kamati. Kamati hii inajukumu la kuidhinisha mpangokazi wa mradi wa mwaka, mkakati wa utekelezaji wa mradi, taarifa za utekelezaji wa mradi na kushauri kuhusu uboreshaji wa utekelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa KAIZEN upo katika awamu ya pili na unatekelezwa kupitia ufadhili wa nchi ya Japan, changamoto ya miradi inayotekelezwa na wafadhili haina *guarantee* ya utekelezaji wake kuendelea. Mipango ya Wizara ya kuiendeleza falsafa ya KAIZEN pindi ufadhili utakapoisha ni kuanza kuwatoza ada wahitaji ili waweze kuuendeleza jambo ambalo litakuwa si jema sana kwa waratibu lakini pia wahitaji wa huduma kwa kuwa walishazoea kuipata bure. Kamati inaishauri Serikali kujipanga kuuendeleza mradi huu kwa fedha zake ili kuonyesha wadau mapenzi/ushiriki wa Serikali katika kujenga na kuimarisha Sekta ya Viwanda.

**Mheshimiwa Spika,** falsafa ya KAIZEN inatekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara, na jukumu la kusimamia kiwanda cha URAFIKI lipo chini ya Wizara hiyo, falsafa hii imevisaidia/nufaisha viwanda vingi na kuhakikisha vinafanya kazi kufikia uwezo wake. Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha kabla awamu ya pili ya utekelezaji wa mradi haijaisha wanakisaidia kiwanda chetu cha URAFIKI.

**Mheshimiwa Spika,** falsafa ya KAIZEN ni nzuri sana imekuwa ikisaidia viwanda vingi lakini inafahamika kwa watu wachache tu. Kamati inaishauri Wizara kuitangaza katika vipindi vya redio na televisheni ili kukuza uelewa wa huduma hii nzuri.

**o) Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Sera zinazosimamia Ujenzi wa Viwanda;-**

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Viwanda na Biashara inasimamia na kuratibu Sera kuu nne (4) ambazo ni Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ya mwaka 1996-2020, Sera ya Maendeleo ya Viwanda vidogo na Biashara ndogo ya mwaka 2003, Sera ya Taifa Biashara ya mwaka 2003 na Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo ya mwaka 2008. Kabla

Sekta ya Uwekezaji kuhamishiwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ilikuwa inasumamia Sera ya Taifa ya Uwekezaji ya Mwaka 1996.

**Mheshimiwa Spika,** Sera hizi mahsusi za usimamizi wa ujenzi wa Tanzania ya Viwanda ni za muda mrefu sana zina umri takribani **miaka 11 hadi 22,** kwa mazingira ya sasa ya biashara zinaonekana kupitwa na muda. Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya sera hizi na kuziboresha ili kuhakikisha zinaendana na mazingira ya sasa ya kufanyia biashara. Sambamba na Sera, Sheria za usimamiza wa biashara pia zimepitwa na wakati haziendani na mazingira ya sasa.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na Sera, Sheria zinazosimamia sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji (hususani sheria zilizounda mamlaka za udhibiti) ni nzuri lakini ziliandaliwa kuendana na mazingira ya biashara ya wakati huo. Kamati inasisitiza Serikali kuzipitiwa upya sheria hizi na kuboresha kwa lengo la kuziwezesha kuendana na mazingira ya sasa ya Biashara.

**Mheshimiwa Spika,** tunazungumzia Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda lakini tunaenda kujenga viwanda ambavyo havitakuwa na uhai mrefu, kinachopelekea kuu viwanda vyetu vya ndani ni gharama kubwa za uzalishaji kuanzia hatua ya uzalishaji mpaka kufika Sokoni. Hatua hii inapelekea bidhaa zinazozalisha nchini kuwa kubwa na kushindwa kushindana katika soko matokeo nchi yetu imekuwa soko la bidhaa kutoka nche. Kamati inaendelea kuisisitiza kuwa kuna haja ya Serikali kukaa chini na wazalishaji wa ndani na kubainisha gharama zao za uzalishaji na Serikali kuangalia namna ya kuwapunguzia mzigo huo, hatua hii itawasaidia wazalishaji wa ndani kuzalisha kwa gharama nafuu na kuweza kushindana katika soko.

p) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2018**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa Mafungu yote Mawili (Fungu **44** na **60**) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **143,334,153,648.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **43,309,628,648.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **100,024,525,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **20,006,300,000.00**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliarifiwa kuwa hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imepokea shilingi **26,703,462,562.00** kwa mafungu yote mawili, kiasi hiki ni sawa na asilimia **18.63** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kati ya fedha zilizopokelewa ni shilingi **6,477,221,314** tu ndio imetolewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, kiasi hichi ni sawa na asilimia **6.47** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Utoaji huu wa fedha za maendeleo haouonyeshi uwiano sawa wa matumizi ya kawadi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inendelea kuishauri Serikali kupeleka kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa lengo la kuziwezesha wizara zetu kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa makusanyo hadi kufikia Disemba, 2018 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **7,900,492,248.00** sawa na asilimia **39.5** ya kiasi ilichoqipangia kukusanya kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mahesabu ya kawaida Wizara ilipaswa kuwa imekusanya asilimia 50 ya lengo iliyokuwa imejipangia lakini imekusanya asilimia **39.5** tu. Kamati inaishauri Serikali kuangalia changamoto

zilizokwamisha kufikia lengo lililokusudia na kuzitatua, hili liende sambamba na kuangalia kama ilijipangia makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya.

## **2.5 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inasimamia na kushauri kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu masuala ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha Machi, 2018 hadi Januari, 2019 ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii. Taarifa hizo ni kama ifuatavyo:-

- a) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Mikakati ya Serikali katika kutekeleza kaulimbiu yake ya Wiki ya Mazingira ambayo ni "Mkaa ni gharama tumia Nishati mbadala".**

**Mheshimiwa Spika**, ripoti ya pili ya Hali ya Mazingira nchini ya mwaka 2014 imebainisha kuwa kasi ya uharibifu wa misitu ni kubwa ambapo kila mwaka zaidi ya hakta 372,000 zinapotea. Moja ya jambo linalochangia upotevu wa misitu kwa kiasi kikubwa ni ukataji wa misitu kwa ajili ya kupata nishati ya kuni na mkaa.

**Mheshimiwa Spika**, Biashara ya kuni na mkaa ni chanzo cha mapato lakini pia inatoa ajira kwa jamii wananchi wanaojihusisha na biashara hiyo. Changamoto inakuja katika zoezi la kuzalisha bidhaa hii ambapo kwa kiasi kikubwa linaendeshwa kinyume na taratibu na sheria za kuendesha biashara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya jamii haziwezi kabisa kuacha matumizi ya kuni na mkaa, na hii ni kutokana na asili ya shughuli zao. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango wa kuzielimisha jamii hizi kuhusu uvunaji endelevu wa misitu yetu kwa ajili ya mkaa, hatua ambayo itakuwa



ya faida kwa wote ambapo Serikali kuendelea kukusanya kodi ya zao la mkaa, wazalisha na wauza mkaa watajipatia kipato na watumiaji watapata bidhaa;

**Mheshimiwa Spika,** aidha, kuna taasisi zisizo za kiserikali (NGO's) mbalimbali zinaunga mkono matumizi ya mkaa, lakini zinahimiza kutumia uvunaji endelevu wa misitu yetu. Kamati inaishauri Serikali kuzitambua taasisi hizo na kufanya nazo kazi katika kusambaza elimu ya uvunaji endelevu.

**Mheshimiwa Spika,** kutegemea gesi ya LPG kama nishati mbadala ni kuwaumiza watanzania kwa kuwa bei ya nishati hii ni kubwa na inaendelea kupanda. Kamati inapongeza mpango wa Serikali wa kutaka kuanza kusindika gesi asili ili iweze kutumika majumbani, utekelezaji wa mpango huu ufanyike haraka ili kuiokoa misitu yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Nishati ya kuni na mkaa ni tegemeo la watu wengi na takwimu zinaonyesha takribani asilimia 90 ya watanzania wanatumia nishati hiyo kutokana na kuwa inapatikana kwa bei nafuu. Kamati inashauri ufanyikie utafiti wa kutosha ili kupata nishati mbadala ambazo zitakuwa za kudumu na bei nafuu, upatikanaji wa nishati mbadala ya bei nafuu itasaidia kupunguza matumizi ya nishati ya mkaa na kuni.

**Mheshimiwa Spika,** kuna matumizi makubwa ya nishati ya mkaa na kuni katika taasisi za Serikali hususani Magereza na shule za bweni nchini jambo linalopelekea ukataji misitu kwa kiasi kikubwa na kupelekea maeneo mengi kuwa na hali ya jangwa. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango mahsusi kwa ajili ya kuzipatia taasisi hizi nishati mbadala ili kuokoa kiasi kikubwa cha miti inayokatwa kwa ajili ya kuni na mkaa. Sambamba na hilo taasisi hizi zihimizwe kuwa na mashamba ya miti, kuzalisha na kutumia biogas na majiko banifu.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria za Uvunaji wa miti zimekuwa kikwazo katika baadhi ya maeneo, mfano mkulima akitaka kusafisha eneo kwa ajili ya kilimo na akavuna miti iliyopo katika eneo hilo, hutozwa tozo kama wavunaji miti ya mkaa. Hatua hii hupelekea baadhi ya wakulima kuamua kuteketeza kwa moto maeneo hayo ili wasikutwe na miti. Kamati inaishauri Serikali kuiangalia tena Sheria hii ili itoe maelekezo ya namna itakavyotumika kwa baadhi ya maeneo.

**b) Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa kupambana na kuenea kwa Hali Jangwa na Ukame.**

**Mheshimiwa Spika,** tafiti zinaonyesha kuwa asilimia 61 ya nchi yetu ya Tanzania ipo hatarini kugeuka jangwa, mikoa iliyoathirika zaidi ni pamoja na Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Manyara na baadhi ya maeneo ya MKoa wa Kilimanjaro. Juhudi za makusudi zinahitajika katika kupambana na hali hii ili kujinusuru na balaa la jangwa na ukame.

**Mheshimiwa Spika,** juhudi za Serikali katika kipambana na balaa la kuenea kwa hali ya jangwa na ukame ni pamoja na kujiunga katika Mikataba mbalimbali inayohusiana na uhifadhi wa Mazingira ambapo kwa sasa Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na imekuwa ikishiriki katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali chini ya Mkataba huu ikiwa ni pamoja na kutekeleza miradi inayolenga matumizi bora na endelevu ya ardhi, kushiriki mikutano ya nchi wanachama na kuandaa mpango kazi wa kitaifa katika kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame.

**Mheshimiwa Spika,** kama nchi mwanachama wa Mkataba huu Tanzania imeweza kunufaika na ufadhili wa kutekeleza miradi na mbalimbali ambapo mpaka sasa tumefanikiwa kutekeleza miradi minne (4) ambayo ni Mradi wa kujenga uwezo wa kitaasisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais-

Mazingira; mradi wa kuokoa maeneo yaliyoharibika ya miinuko ya Kilimanjaro; Mradi wa kuhifadhi Misitu ya Miomboi Tabora na Katavi; na program ya kuandaa shabaha ya kuzuia uharibifu wa ardhi. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuridhia kuwa Mwanachama wa Mkataba huu muhimu ambao umetuwezesha kupata manufaa.

**Mheshimwa Spika,** kwa nia ya kupunguza athari ya kuenea kwa hali ya jangwa na Ukame. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ambapo itabainisha kila aina ya shughuli itakayofanyika katika eneo husika na jamii zijengee uelewa juu ya matumizi bora ya ardhi. Sambamba na hilo Serikali iongeze juhudi katika kulinda maeneo yaliyohifadhiwa kama ardhi owevu, misitu, mbuga za wanyama na mapori endelevu. Aidha, jamii ipatiwe elimu juu ya faida zipatikanazo katika kuhifadhi maeneo husika, hatua ambayo itazifanya jamii kuwa miongoni mwa walenzi wa hifadhi hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina faida ya kuwa na maeneo mengi yaliyohifadhiwa lakini pia zinafanyika jitihada kubwa za kutunza mazingira, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango wa kutambua fedha na nguvu kazi (*shadow pricing*) inayotumika katika maeneo ya hifadhi, ili kubainisha juhudi za nchi katika kupambana na hewa ukaa jambo litakalotuwezesha kupata ufadhili zaidi kutoka katika mifuko ya usimamizi wa mazingira ya Dunia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kampeni za Serikali za Upandaji miti zitekelezwe kwa kuzingatia maeneo yaliyoathirika zaidi na ukame lakini pia miti inayopandwa izingatie asili ya eneo husika ilikupata matokeo mazuri. Sambamba na hilo Serikali ifuatilie miradi ya maji iliyoanzishwa kwa ajili ya umwagiliaji vitalu hatua hii itasidia ufanisi wa Kampeni hizi.

**Mheshimiwa Spika,** katika kuilinda misitu yetu Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira ishirikiane na Wizara yenye dhamana ya misitu kuandaa mpango wa usimamizi na uvunaji wa misitu yetu, pia kutengwa maeneo ya hifadhi na maeneo ya kuvuna miti.

- c) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kuhusu Juhudi za Kuhifadhi Ziwa Manyara na Ziwa Jipe ambayo yapo katika hatari ya kutoweka.**

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imeneemeka takribani asilimia 10 ya eneo la nchi yetu limefunikwa na ardhi owevu ambayo inajumuisha maziwa, bahari, mito, mabwawa n.k. Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 1997 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namba 20 ya Mwaka 2004 zinaelekeza na kusisitiza umuhimu wa kutunza na kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Maziwa, Mito, Mabwawa pamoja na vyanzo vya maji kwa kushirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali ikiwemo jamii. Serikali za Mitaa zimepewa wajibu wa kuhakikisha rasilimali maji zilizopo katika maeneo yao zinalindwa na kutunzwa.

**Mheshimiwa Spika,** maziwa ikiwemo ziwa Manyara na Jipe yana manufaa makubwa ambayo ni pamoja na kuboresha afya na kipato cha wakazi wa eneo linalozunguka ziwa kwa shughuli za uvuvi; kuboresha hali ya hewa na kuleta mandhari nzuri; ardhi ya kando kando ya ziwa huwa na rutuba nyingi hivyo kuvutia shughuli za kilimo; na pia wanyama, ndege na bioanuai zinazopatikana katika maeneo ya maziwa huvutia shughuli za utalii hivyo kuchangia katika pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na manufaa yapatikanayo katika maeneo ya hifadhi za maziwa lakini bado kuna uharibifu mkubwa unaofanyika kutokana na shughuli za binadamu za kiuchumi (mfano Uvuvi, Kilimo

kuzunguka eneo la ziwa na vyanzo vya maji vya ziwa, unyweshaji wa mifugo n.k). Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya utoaji elimu kwa jamii wanaozunguka maeneo ya hifadhi za maziwa kuhusu ya athari za kuharibu mazingira hayo, pia jamii ifundishwe namna bora ya utekelezaji wa shughuli zao bila kuathiri hifadhi ya maziwa pamoja na vyanzo vyake vya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Ziwa Manyara na Jipe yanapatikana katika mipaka ya nchi yetu na nchi ya Kenya lakini jitihada za uhifadhi wa maziwa haya zinaonekana kuwa za upande mmoja yani Tanzania tu. Kamati inaishauri Serikali kukutana na nchi husika na kurejea makubaliano ya Uhifadhi waliyowekeana kwa lengo la kuongeza uhifadhi wa maziwa haya.

**Mheshimiwa Spika,** asilimia 51 ya ziwa Manyara ipo katika hifadhi ya Taifa na 49 iliyobaki ipo katika usimamizi wa Serikali za Mitaa ambao wameonekana kutotilia uzito uhifadhi wa sehemu waliyopewa. Kamati inashauri Serikali kubadilisha umiliki huo na asilimilia 100 ya eneo la Manyara zote ziwewe chini ya hifadhi kwa kuwa Halimashauri haijalipa kipaumbele uhifadhi wa sehemu ya Ziwa waliyoachiwa.

d) **Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Basel kuhusu Udhhibiti wa Usafirishaji na Utupaji wa Taka za Sumu.**

**Mheshimiwa Spika,** ongezeko la uzalishaji taka hatarishi na zenye sumu katika nchi zenye viwanda kulipelekea uhitaji wa kuwa na utaratibu wa kudhibiti usafirishaji wa taka hizo na utupaji wake kwa namna ambayo haina madhara kwa mazingira, watu na viumbe wengine. Majadiliano yalifanyika chini ya Umoja wa Mataifa na hatimaye mkataba wa Basel ulipitishwa. Mkataba wa Basel unahusu Udhhibiti wa Usafirishaji wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na utupaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** madhumuni ya kuanzishwa kwa Mkataba huu ilikuwa ni kwa ajili ya kulinda afya ya binadamu na mazingira kwa kudhibiti uzalishaji, usafirishaji na utupaji wa taka zenye sumu. Kwa nchi ya Tanzania Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kwa kushirikian ana Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira - *NEMC* pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ndio inasimamia utekelezaji wa Mkataba huu ambapo kila mmoja amepewa majukumu yake kuhusiana na utekelezaji wa mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya teknolojia yamewezesha urejeleshaji wa taka hatarishi kwa lengo la kupata malighafi au kuongeza thamani na kupata mali nyingine hatua ambayo imechochea kwa kiasi kikubwa ukusanyaji, usafirishaji na biashara ya taka ikiwemo chuma chakavu, betri mbovu, mafuta na vifaa chakavu vya kielektroniki. Hivyo hatua ya Serikali ya kuridhia mkataba huu ilikuwa njema ukizingatia nchi yetu bado haijawa na miundombinu na teknolojia ya urejeleshaji wa taka hatarishi.

**Mheshimiwa Spika,** usimamizi wa taka hatarishi hapa nchini unakabiliwa na changamoto ikiwemo uelewa mdogo wa wadau wanaojihusisha na ukusanyaji, utunzaji na usafirishaji wa taka hizo. Madhara yanayopatikana kutokana na *kumis-handle* taka hizi ni makubwa, Kamati inaishauri Serikali kutoa elimu kwa wadau wanaojishughulisha na shughuli hizo ili kuinusuru nchi na madhara yanayoweza kupatikana.

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu bado haina miundombinu na teknolojia ya urejeleshaji wa taka hatarishi jambo ambalo tunalazimika kuzisafirisha nje ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Uwekezaji kutafuta wawekezaji ambao watakuwa tayari kuwekeza katika shughuli za urejeleshaji wa taka hatarishi hatua ambayo itatusaidia kupunguza gharama za kuzisafirisha nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza jitihada za Serikali za kuwa mwanachama wa mikataba mbalimbali ya uhifadhi wa Mazingira, lakini inatoa angalizo kwa Serikali kuhakikisha nchi inapata manufaa stahiki yatokanayo na mikataba hiyo. Serikali ipitie upya mikataba yate iliyowahi ingia kisha kuandaa mpango mkakati wa kuitekeleza kwa manufaa ya nchi.

- e) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira katika Ngazi ya Serikali za Mitaa; na Changamoto zilizopo katika Utekelezaji na Usimamizi wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na mikakati ya kuzikabili.**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ilipitishwa na Bunge Mwaka 2004 na kupewa jukumu la kuweka mfumo wa kitaasisi ambao utakuwa na mipango endelevu ya kutunza na kuhifadhi mazingira. Sheria hii inatamka kuwa mazingira ni urithi wa kizazi kilichopo na vijavyo na inampa kila mtu anayeishi Tanzania haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 imebainisha majukumu na wajibu wa kila Sekta na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia masuala ya Uhifadhi wa Mazingira. Aidha, Sheria hii imezielekeza Halmashauri za Jiji, Manispaa, Wilaya na Mji kuteua au kuajiri Ofisa Usimamizi wa Mazingira ambaye ndio huwa msimamizi mkuu wa masuala ya mazingira katika eneo husika.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisa Mazingira ambae ni muajiriwa katika ngazi ya Serikali za Mitaa amepewa majukumu ya kusimamia masuala yote ya mazingira katika eneo lake na kuhakikisha yanatekelezwa kwa kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Pia Sheria inamuelekeza kushauri Kamati ya Usimamizi wa Mazingira ya eneo lake kuhusu masuala yote ya

mazingira; kuandaa taarifa kuhusu hali ya mazingira ndani ya eneo husika; na Kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Mazingira na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC kuhusu utekelezaji wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira unakumbana na changamoto mbalimbali ikiwemo uhaba wa watumishi hasa wa fani ya Maafisa Mazingira; masuala ya usimamizi wa mazingira katika ngazi ya serikali za mitaa kutopewa umuhimu na kuchukuliwa kama kufanya usafi; Bajeti kidogo inayotengwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika shughuli za Mazingira; Uelewa mdogo wa wananchi na watendaji katika ngazi mbalimbali juu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira; Upungufu wa vitendea kazi ambao hukwamisha shughuli za uratibu wa kazi mazingira; Ushiriki mdogo wa Serikali za Mitaa katika kuandaa mipango ya hifadhi ya mazingira na usimamizi wa Sheria ya mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** jamii inaelewa mdogo juu ya umuhimu wa utunzaji mazingira jambo linalopelekea ukiukwaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwa kiasi kikubwa. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiwezesha Ofisi ya Makamu Rais-Mazingira kirasilimali fedha na watu ili waweze kuwafikia watazania wengi na kuwapatia elimu ya Uhifadhi wa Mazingira (faida za kuyatunza na Hasara ya kuyaharibu) kwani kwa sasa uelewa wa jamii nyingi kuwa kufanya usafi tu ndio kutunza mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya utekelezaji wa Sheria ya Mita 60, baadhi ya maeneo yameathiriwa na Mabadiliko ya Tabia nchi hivyo kusababisha vyanzo vya maji kusogea mpaka kwenye maeneo ya wakazi au wanapoendeshea shughuli zao za kijamii. Kamati inaishauri Serikali kupitia NEMC na Wizara ya Maji kutafuta ufumbuzi wa haraka wanamna ya kutekeleza Sheria ya Mita 60 kwa lengo la kuondoa migogoro iliyopo lakini pia kuwanusuru watu ambao maeneo yao yamefikwa na vyanzo vya maji kutokana na Mabadiliko ya Tabianchi;



**Mheshimiwa Spika,** shughuli za uchimbaji madini zimekuwa zikichafua mazingira kwa kiasi kikubwa ndio maana Sheria ya Madini iliweka kifungu ambacho kinamlazimu muwekezaji kutenga fedha kwa ajili ya kurejelesha mazingira ya mgodi baada ya kufungwa. Changamoto ni fedha zilizotengwa hupokelewa na kuratibiwa na Wizara ya Nishati ambayo si Wizara yenye dhamana ya usimamizi wa Mazingira, na mwisho wa siku kutumika kinyume na malengo yaliyokusudiwa. Kamati inashauri fedha hizo zipelekwe kwa Wizara yenye dhamana ya Mazingira, sambamba na hili sheria za ufungaji wa migodi iwekwe kipengele kinachotoa fursa kwa wakazi wa eneo husika kushirikishwa/kushauri katika zoezi la kufunga mgodi ambapo watashauri nini kifanyike katika eneo lao kwa kuzingatia shughuli za maendeleo za eneo husika;

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Taifa ya Mazingira ni ya Mwaka 1997 takribani miaka 22 ambapo kuna mambo mengi yamekwishatokea na hayakuhusiswa kwenye Sera hii (mfano mabadiliko ya Tabia nchi na viumbe vamizi). Sambamba na hilo Sera hiyo inatekelezwa kutumia Sheria ya mwaka 2004 ambayo imehusisha mabadiliko mbalimbali ambayo hayapo kwenye Sera. Kamati inaishauri kufanya mapitio ya Sera ye Taifa ya Mazingira na kuihuisha ili iendane na hali halisi ya mazingira kwa sasa.

f) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utendaji wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (National Environmental Management Council –NEMC)**

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ni taasisi ya Serikali inayotekelaza majukumu yake chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Baraza hili lilianzishwa chini ya Sheria Namba 19 ya Mazingira mnamo mwaka 1983 ambapo ilikuwa na jukumu la kutoa ushauri kwa Serikali na wadau kuhusu masuala ya Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kutungwa kwa Sheria ya Usimamizai wa Mazingira ya Mwaka 2004 majukumu ya baraza yalihuwishwa na kuwa ni kuratibu utekelezaji wa sera na sheria ya mazingira katika Nyanja kuu nne ambazo ni kutekeleza shughuli za uzingatiaji na usimamizi wa mazingira; kusimamia mchakato wa tathimini ya athari za mazingira; kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya maamuzi yanayohusu mazingira; na kusimamia kwa ujumla mambo yote yanayohusu mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa Majukumu yake Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira linakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watumishi wenye fani ya mazingira katika Baraza ukilinganisha na majukumu ya baraza kitaifa; uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sheria za mazingira jambo linalopelekea kutokuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za mazingira; na ushirikiano mdogo wa wadau wengine katika kusimamia utekelezaji wa sheria ya mazingira wakati sheria hiyo imempa kila mdau majukumu yake;

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira linadhamana kubwa ya kusimamia na kuratibu shughuli za utunzaji wa mazingira lakini kuna baadhi ya maamuzi ni lazima yafanywe na Waziri mwenye dhamana. Kamati inashauri NEMC wapewe mamlaka kamili, badala ya kuwa Baraza iwe Mamlaka ya Taifa ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira, hatua hii itaipaa mamlaka kamili ya kusimamia masuala ya Mazingira na pia tutampunguzia Waziri majukumu.

**Mheshimiwa Spika,** wawekezaji wengi huwa hawaweki uzito katika suala la vibali vya mazingira, huanza kutafuta vibali hivi dakika za mwisho wakati ambapo wamesha pata vibali vingine vya uwekezaji na kutegemea kupata cheti cha mazingira kwa muda mfupi jambo ambalo haliwezekani kwa kuwa EIA ni mchakato mrefu kidogo. Kamati inaishauri Serikali kupitia mamlaka zake zinazoratibu uwekezaji, kuwashauri Wawekezaji kufuatilia

kibali cha mazingira sambamba na vibali vingine ili kutoa nafasi kwa mchakato wa EIA kukamilika;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kukasimisha jukumu la kusaini na kutoa vyeti cha EIA kwa NEMC ambao ndio wasimamizi wakuu wa zoezi hili, kwa sasa cheti ni mpaka kinasainiwa na Waziri mwenye dhamana ya mazingira ambae anamajukumu mengine mengi;

**Mheshimiwa Spika,** mipango miji yetu ni ya zamani sana jambo ambalo linaleta mgongano katika matumizi ya ardhi, kuna baadhi ya maeneo viwanda vimejengwa katika makazi na kwingine makazi yamejengwa maeneo ya Viwanda, na maeneo mengine machinjio yapo katika maeneo ya makazi. Kamati inaishauri Serikali kuipitia upya ramani za mipango miji na kuiboresha kwa lengo la kuondoa migogoro inayoendelea;

**Mheshimiwa Spika,** maeneo mengi nchini hayana vituo vya kuteketeza taka hatarishi jambo ambalo linalazimu wazalishaji taka hizo kuzisafirisha mpaka Dar es Salaam jambo ambalo si salama kwa kuwa zimekuwa zikianguka mabarabarani na kuhatarisha afya za wapiti njia. Kamati inaishauri Serikali kupitia NEMC kushawishi wawekezaji wengi zaidi kuwekeza katika maeneo mengi zaidi ili kuondoa hii adha ya kuzisafirisha kwenda Dar es Salaam;

g) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Changamoto za Viumbe Wageni vamizi katika Mazingira**

**Mheshimiwa Spika,** Viumbe Wageni/Vamizi ni Kiumbe chochote kigeni katika mazingira ambacho uwepo wake huleta madhara kwa mazingira, uchumi, baionuai, afya ya jamii, mifugo na mimea. Chanzo cha Viumbe vamizi ni Shughuli za kibinadamu ambazo huwaleta viumbe maeneo mapya, shughuli hizo ni pamoja na majaribio ya mazao ya kilimo, misitu na mifugo; mizunguko ya mifugo toka eneo moja na jingine; mabadiliko ya tabianchi; viumbe kubadili tabia kukabiliana na mabadiliko yeyote;

maendeleo ya mifumo ya usafiri duniani (mf. Safari za meli); na Mifumo ya asili kama Upepo.

**Mheshimiwa Spika,** madhara ya Viumbe Vamizi yameanza kuonekana tena kwa kasi katika Mazingira, madhara hayo ni pamoja na kupungua kwa bionuai na kuharibu vyanzo vya maji; kiuchumi hupunguza uzalishaji kilimo na kuathiri shughuli za utalii; kiafya na jamii husababisha kuenea magonjwa na kupunguza uzalishaji chakula. Kamati inaishauri Serikali kufanya utafiti wa kina na kubaini Viumbe wageni/vamizi waliopo nchini na maeneo wanapopatikana, hatua hii itatoa picha ya ukubwa wa tatizo na kujipanga namna ya kulitatua;

**Mheshimiwa Spika,** Kuna baadhi ya mimea ni migeni na vamizi lakini yaweza kuwa na faida, Kamati inashauri Serikali ifanye utafiti kuhusu mimea hii vamizi na kubaini faida na madhara yake kisha ndio ifanye uamuzi wa kuyateketeza;

**Mheshimiwa Spika,** Kuna baadhi ya viumbe wageni/vamizi ambayo athari zake katika mazingira zimekwishaonekana na zinaenea kwa kasi sana mfano gugu karoti ambalo pia ni sumu, Kamati inashauri zichukuliwe hatua za haraka katika kuteketeza mmea huu;

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa nchi haina mpango mkakati wala miongozo ya kushughulikia changamoto ya Viumbe vamizi jambo linalopelekea ugumu kutatua changamoto hii. Kamati inatambua kuwa kuna kikosi kazi kimeundwa kwa ajili kushughulikia changamoto ya viumbe wageni vamizi, Kamati inaomba kushirikishwa kabla taarifa hiyo kabla haijawa *final* kwa lengo la kushauri tu.

- h) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Uhifadhi wa maeneo lindwa kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira; na Jitihada za Serikali katika kuyahifadhi maeneo lindwa.**

**Mheshimiwa Spika,** takribani asilimia 30 ya eneo la nchi hii imehifadhiwa kisheria kwa namna moja ama nyingine, maeneo hayo yanajumuisha mbuga za taifa, mapori ya akiba ya wanyama pori, hifadhi ya bahari, misitu ya akiba.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya mazingira sura ya 191 katika kusimamia maeneo lindwa imempa Waziri mwenye dhamana ya mazingira mamlaka kutangaza eneo lolote la ardhi linaloweza kuharibika upesi kiikolojia au eneo nyeti, kuwa eneo lindwa lakini anapaswa kuzingatia mapendekezo ya Kamati ya Taifa ya Ushauri ya Mazingira. Sheria hii pia imeweka usimamizi wa maeneo lindwa chini ya Mamlaka ya Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** manufaa ya kuanzisha maeneo lindwa au nyeti ya Mazingira ni pamoja na kukuza na kuboresha sekta ya utalii, vyanzo vya maji na umeme, hifadhi ya bioanuai (wanyama, wadudu, ndege)

**Mheshimiwa Spika,** Sheria za kusimamia maeneo lindwa zinajitosheleza sana tatizo lipo katika usimamizi wa maeneo hayo, ambao unasababishwa na ufinyu wa rasilimali fedha na watu. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya wizara hii muhimu na kutoa vibali vya kuajiri maafisa mazingira wenye taaluma ya mazingira kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mazingira unadhamana ya kubwa ya kusimamia mazingira lakini unakumbana na changamoto ya fedha, Kamati inaishauri Serikali kuuwezesha mfuko wa mazingira na kuupatia kibali cha

kukusanya asilimia chache ya tozo zinazohusiana na mazingira, kuimarika kwa Mfuko huu kutaiwezesha Wizara ya Mazingira kutekeleza majukumu yake bila kutegemea fedha kutoka mfuko mkuu wa Serikali;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuzieliisha jamii juu ya uhifadhi wa maeneo lindwa, lakini elimu hii izingatie wahusika wa eneo, aina ya maisha na shughuli wanazofanya ukihusianisha na aina ya uharibifu wa mazingira wanaoufanya ili kuhakikisha wanapata elimu stahiki (mkulima, Mfugaji, mvuna mkaa hawa wanafanya shughuli tofauti na utaribifu tofauti) hatua hii itasaidia kupunguza migogoro inayotokea kati ya maafisa mazingira na jamii;

**Mheshimiwa Spika,** kuna baadhi ya maeneo lindwa yapo katika umiliki wa watu Binafsi (mfano eneo la kuzunguka ziwa Chale hivyo faida za utalii katika ziwa chale zinaenda kwa mtu binafsi) na Wizara yenye mamlaka ya kusimamia mazingira hana mamlaka ya kuingia katika maeneo hayo. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha maeneo yote ya Vivutio na Lindwa yanawekwa chini ya Umiliki wa Serikali ili kuhakikisha manufaa ya maeneo hayo yanakuwa ya nchi na sio watu binafsi.

i) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Muongozo wa Taifa wa Tathimini ya Mazingira kimkakati (SEA).**

**Mheshimiwa Spika,** Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) ni utaratibu wa kuhusisha au kutathimini masuala ya mazingira ili kuleta dhana ya uendelevu katika ngazi ya miswada, kanuni, sera, mikakati, progamu na mipango ikihusisha masuala ya usimamizi wa mazingira. Utaratibu huu ulianzishwa miaka ya 1960 baada ya mapinduzi ya Viwanda, kwa Tanzania ulianza kutumika rasmi baada ya kuanzishwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 kabla ya hapo TMK ilikuwa inafanyika kihiyari tu.

**Mheshimiwa Spika,** mwongozo wa Tathimini ya Mazingira Kimkakati unaelekeza hatua na ngazi mbalimbali za kufuatwa katika kusimamia TMK lengo likiwa ni kuhakikisha masuala ya mazingira yanajumuishwa mapema katika mipango ya maendeleo ili kuleta maendeleo endelevu na kubainisha fursa na vikwazo vinavyoweza kuathiri au kuathiriwa na sera, miswada, kanuni, mikakati, mipango na program.

**Mheshimiwa Spika,** kuna umuhimu mkubwa wa kufanya Tathimini ya Mazingira Kimkakati kwani husaidia kutambua mibadala ya maendeleo mapema na kutoa miongozo stahiki katika hatua ya sera, miswada, mipango na mikakati; kushirikisha wadau wote katika hatua ya mwanzo ya mipango ya maendeleo; kuwezesha ushirikiano wa nje ya mipaka ya nchi katika usimamizi wa maliasili za pamoja;

Tathimini ya Mazingira Kimkakati pia inaweza kusaidia kutambua na kushughulikia maeneo yanayoweza kuwa na migogoro au utofauti katika hatua za awali za kutunga sera mpya, miswada, kanuni, mikakati, mipango na programu; na hivyo kuzuia makosa yatakayogharimu.

**Mheshimiwa Spika,** kufanya Tathimini ya Mazingira Kimkakati ni takwa la kisheria, kifungu Namba. 104 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kinaelekeza wakati wa kuandaa muswada ambao una uwezekano wa kuwa na athari katika usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira au usimamizi wa endelevu wa maliasili TMK inapaswa kufanyika na kuwasilishwa kwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Sambamba na hilo, kifungu Namba 105 kinalekeza kufanya TMK katika maliasili ya madini, petrol, vituo vya kufua umeme wa maji na miradi mikubwa ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kuwa na Tathimini ya Mazingira Kimkakati ni kuhakikisha kunakuwa na ushiriki wa kipengele cha uhifadhi wa mazingira katika hatua za awali za utekelezaji wa miradi mbalimbali ambayo kwa namna moja ama nyingine itahusisha masuala ya mazingira

(hususani miradi mikubwa ya maendeleo). Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha miradi yote mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali inapitia hatua za Tathimini ya Mazingira Kimkakati kwa lengo la kuhamasisha wadau binafsi kutekeleza TMK.

j) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa Nchini;**

**Mheshimiwa Spika,** Bioteknolojia ya Kisasa (Third generation biotechnology) - ni teknolojia inayohusisha uhamishaji wa viini tete/vinasaba vya uhai kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine kisichohusiana nacho kinasaba (genetic engineering) yani jeni inaweza kuhamishwa kutoka Samaki kwenda Mimea au Kuku kwenda Nyanya.

**Mheshimiwa Spika,** Bioteknolojia ya Kisasa inaweza kutumika katika sekta mbalimbali kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuleta tija kwa maendeleo endelevu. Mfano inaweza tumika katika sekta ya kilimo kuongeza uzalishaji na uboreshaji wa mazao ya kilimo; sekta ya afya kwa kutengeneza madawa na chanjo; viwandani katika kutengeneza bidhaa zinazotokana na viumbe au sehemu za viumbe pia katika kufanya urejeshaji wa taka sumu za viwandani kabla ya kuziruhusu kutupwa.

**Mheshimiwa Spika,** athari zinazoweza kutokana na matumizi ya GMOs ni pamoja na uharibifu wa bioanuai na uoto wa asili wanaotumika katika majaribio; usugu wa dawa kwa matibabu ya magonjwa; kujitokeza kwa magugu na wadudu sugu; na kupotea kwa mbegu za asili.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais mratibu namsimizi wa masuala yote yanayohusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa nchini. Katika kutekeleza hilo Ofisi hutoa elimu kwa umma na kujenga uwezo wa wataalam na taasisi za utafiti na udhibiti, kusimamia usalama wa utafiti na usafirishaji wa bidhaa /mazao yanayotokana na bioteknolojia ya kisasa.



**Mheshimiwa Spika,** uwezo wa nchi katika kudhibiti madhara yatokanayo na teknolojia hizi bado ni mdogo, Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika kuingia mikataba ya uingizaji wa bioteknolojia mpya nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa nchi inakabiliwa na changamoto ya viumbe vamizi ambao wengi wa viumbe hivyo chanzo chake ilikuwa ni haya majaribio ya bioteknolojia. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini sana katika kuridhia bioteknolojia zinazolingia nchini kuwa lengo la kuepuka kufanywa nchi ya majaribio ya teknolojia hizi.

k) **Kupokea na kujadai Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Usimamizi wa Mazingira katika Sekta ya Mafuta na Gesi.**

**Mheshimiwa Spika,** nishari ya gesi na mafuta ni nyenzo muhimu sana katika maendeleo ya uchumi wanchi, nchi yetu imebarikiwa rasilimali ya gesi ambapo ugunduzi uliofanyika katika maeneo mbalimbali umebaini akiba ya futi za ujazo 55.098 trilioni ya gesi asilia. Gesi asilia ni nishati rafiki wa mazingira na inaweza kutumika kama nishati mbadala wa kuni, mkaa, pamoja na mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya nishati ya gesi yakisimamiwa vizuri yatachangia sana kwenye hifadhi ya mazingira. Hatua hii itasaidia kupunguza ukataji wa misitu kwa ajili ya mkaa, uzalishaji wa gesi zinazochangia uchafuzi wa hewa utapungua hatimaye mabadiliko ya tabianchi yatafungua.

**Mheshimiwa Spika,** Baraza limepewa mamlaka na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 ya kufanya ukaguzi, utafiti na uchunguzi utakaosaidia katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira. Kwa muktadha huo NEMC ndio chombo tunachokitegemea katika kusimamia masuala ya mazingira katika sekta ya gesi na mafuta.

**Mheshimiwa Spika**, NEMC inashindwa kusimamia kikamilifu sekta ya Gesi kwa kuwa haina utaalamu na wataalamu katika sekta ya mafuta na gesi (TAM). Pia, changamoto ya upungufu wa vitendea kazi kwa ajili ya kufanya uperembaji na ufinyu wa rasilimali fedha jambo linalosababisha ishindwe kuasimamia Sekta ya gesi kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Mafuta na Gesi ni sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika uchumi wa nchi, lakini kama zisiposimamiwa na kuratibiwa kiukamilifu katika hatua ya uziduaji ni sekta zinazoharibu mazingira kwa kasi. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha NEMC kutekeleza jukumu la kusimamia Sekta ya Mafuta na gesi kwa kuwajengea uwezo wa kitaasisi (wataalamu na utaalamu), rasilimali fedha na vitendea kazi ili waweze kusimamia sekta hii kikamilifu.

**l) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2018.**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira katika Mwaka wa Fedha **2018/2019** waliidhinishiwa shilingi **8,118,494,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **3,524,540,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **4,593,954,000.00** ni matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2018 nusu ya Mwaka wa Fedha **2018/2019** ni shilingi shilingi **5,020,282,003.28** ambapo shilingi **4,481,482,003.00** zilitolewa kwa ajili ya Mishara na matumizi mengineyo na kiasi kilichobaki shilingi **538,800,000.00** ndio ilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya inayotengwa kwa ajili ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira haitoshi kupambana na uharibifu wa mazingira ambao umendelea kufanyika hususani changamoto ya Mabadiliko ya Tabianchi. Aidha, bajeti hii ndogo imeendelea kupungua mwaka hadi

mwaka jambo linaloashiria Serikali yetu kutotoa umuhimu kwa suala la uhifadhi wa mazingira. Kamati kuishauri Serikali kutoa uzito unaostahili katika suala la uhifadhi wa mazingira na ianze kwa kutenga fedha za kutosha za usimamizi wa mazingira na fedha hizo zitolewe kwa wakati.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

#### 3.1 Sekta ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi chote cha kuanzia Machi, 2018 hadi Januari 2019 Kamati ilitekelza majukumu yake ya kikanuni katika kuzisimamia Wizara pamoja na Taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati. Sasa naomba nitumie fursa hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati na niliombe Bunge lako Tukufu liazimie kuwa Maazimio ya Bunge.

##### 3.1.1 Upokeaji wa Fedha kutoka Hazina

**KWA KUWA**, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa hakuna mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina,

**NA KWA KUWA** hali hiyo huchangia kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hususani Miradi ya Maendeleo,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kujipangia Bajeti inayoakisi makusanyo halisi ya Nchi. Sambamba na hilo Kamati inashauri Serikali kujipangia miradi michache ambayo itatekelezwa kwa wakati na kuanza nufaika na miradi hiyo kuliko kuwa na miradi mingi ambayo huishia kupatiwa fedha kidogo kidogo na utekelezaji wake unakuwa hauna tija.

##### 3.1.2 Mradi wa Chuma wa Liganga na Mradi wa Makaa ya mawe wa

###### Mchuchuma

**KWA KUWA** utekelezaji wa Miradi hii umekuwa ukisuasua na kuchukua muda mrefu sana,

**NA KWA KUWA**, Serikali imeonyesha wasiwasi katika mikataba ya uwekezaji kwenye miradi hii,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kutafuta mbobezi (*expert*) ambaye atafanya utafiti katika eneo la mgodi kwa lengo la kubaini aina ya madini, kiasi cha madini kilichopo na thamani ya miradi. Utafiti huo utaipatia Serikali

taarifa ambazo zitaiongoza wakati wa kuingia mikataba ya utekelezaji wa miradi hii. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuwa na mawazo tofauti ya utekelezaji wa Miradi hii, ambapo inaweza kufikiria kuuza chuma kama malighafi au kumtafuta muwekezaji atakaejenga kiwanda cha uchenjuaji.

Sambamba na hilo Kamati inaishauri Serikali kuonyesha nia yake ya kutekeleza miradi hii kwa kuanza walau kujenga miundombinu itakayoweza kufika katika eneo la mradi.

### **3.1.3 Mradi wa Kufufua Kiwanda Cha General Tyre**

**KWA KUWA**, utekelezaji wa mradi wa kufufua kiwanda cha General tyre umechukua muda mrefu (miaka kumi) na Serikali imekwisha weka fedha nyingi lakini hakuna ambacho kinaonekana kufanyika,

**HIVYO BASI**, Bunge linataka kujua kama Serikali imeshapata utaratibu mzuri wa kufufua kiwanda hicho na lini kiwanda kitafufuliwa na kufanya kazi. Sambamba na hilo Bunge linashauri kama hakuna utaratibu ambao uko tayari kwa ajili ya kukufufua kiwanda hicho ni vema eneo la kiwanda lingetumika kuendesha shughuli nyingine za uwekezaji ukizingatia eneo la kiwanda ni eneo lenye mvuto wa kibiashara (*prime area*).

### **3.1.4 Shirika la Maendeleo la Taifa – NDC**

**KWA KUWA** NDC imepewa majukumu ya kusimamia miradi mingi ya maendeleo hasa ile ya kimkakati ambayo utekelezaji wake utachochea ukuaji wa sekta mbalimbali,

**NA KWA KUWA**, Shirika hili muhimu limekuwa likipangiwa na kupatiwa bajeti ambayo haiakisi mahitaji yake halisi,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri NDC kwa kiasi kidogo cha fedha inachotengewa na kupatiwa ni vema katika kila Mwaka wa Fedha ikaamua kujikita na mradi mmoja ili kuutekeleza kikamilifu.

### **3.1.5 Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo - SIDO**

**KWA KUWA** Serikali imeonyesha nia nzuri ya kutaka kuwashirikisha wazawa katika kujengwa uchumi wa Viwanda, watazania wameitikia wito wa Serikali yao lakini wengi wao bado ni wajasiriamali wadogo,

**NA KWA KUWA**, Shirika la Viwanda vidogo – SIDO ndio limepelewa jukumu la kuweka mazingira ya msingi ya kukuza viwanda vidogo na biashara ndogo,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali

- a) Kulingezea nguvu Shirika hili ili kuhakikisha huduma zake kuanzia elimu ya uzalishaji, masoko pamoja na mitaji vinapatikana na kuwanufaisha watazania wengi zaidi kwa lengo la kuongeza ushiriki wao katika ujenzi wa uchumi wa nchi badala ya kutegemea wawekezaji kutoka nje tu; na
- b) Kuziwezesha karakana za SIDO kupata teknolojia mpya kwa lengo la kuzalisha mashine zinazoendana na mahitaji halisi ya soko ya sasa.

**Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo Bunge linataka kujua kama Serikali lilifanya utafiti na kubaini kuwa mahitaji ya sasa katika maeneo ya SIDO ni kujenga mabanda (*shades*). Maana kuna baadhi ya maeneo *shades* hizo zimekuwa zikitumika kama magodauni kinyume na lengo lililokusudiwa, (mfano SIDO Iringa).

### **3.1.6 Utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo Wa Udhhibiti Wa Biashara Nchini**

**KWA KUWA** Serikali imeiaminisha Kamati pamoja na wafanyabiashara kuwa suluhisho la changamoto zote zinazoonekana na kusababisha mazingira ya kufanyia biashara kuwa magumu litapatikana katika Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara Nchini (*Blueprint for Regulatory Reforms To Improve the Business Environment*), ulioandaliwa na Serikali,

**NA KWA KUWA** mpango huo pamoja na mpango kazi wa utekelezaji wake vimekamilika,

**HIVYO BASI** Kamati linashauri Serikali kuanza utekelezaji wa mpango huu haraka iliwekanavyo. Sambamba na hilo Serikali ipange muda maalumu (*time*

*frame*) ya utekelezaji wa mpango huu kwa lengo la kupima ufanisi wake na kuainisha changamoto ambazo zimetatuliwa baada ya kipindi hicho kupita.

### **3.1.7 Mazingira ya Kufanyia Biashara Nchini**

**KWA KUWA**, mfumo wowote wa Uzalishaji unamlenga mlaji wa mwisho (*final consumer*),

**NA KWA KUWA**, mazingira ya kufanyia biashara yamekuwa magumu na ugumu huo kwa kiasi kikubwa unasababishwa na utekelezaji wa sheria za kodi ambazo nyingi tumezinakili kutoka kwa wenzetu walioendelea na haziendani na mazingira yetu,

**NA KWA KUWA** hali hiyo imepelekea baadhi ya wafanyabiashara kuendelea kufunga biashara jambo ambalo halitoi taswira nzuri kwa ustawi wa watazania lakini pia wawekezaji nchini,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuzipitia upya na kuziboresha sheria za kodi ili ziweze kuendana na mazingira halisi ya nchini kwetu, hatua hii itachoche uwekezaji lakini pia itasaidia kumlinda mlaji.

### **3.1.8 Uwepo wa Bidhaa Feki Sokoni,**

**KWA KUWA**, uwepo wa bidhaa feki sokoni unadhihirisha kuwa nchi bado haijafanikiwa kulinda mipaka yake na watendaji wasio waaminifu wanaendelea kufanya vitendo vya rushwa,

**NA KWA KUWA** Serikali ilitambua madhara ya bidhaa feki na kuamua kuanzisha Mamlaka za Udhibiti ambayo zina dhima ya kudhibiti na kuthibiti ubora wa bidhaa kutoka sehemu mbalimbali za ndani na nje ya nchi na kuleta ushindani sawa sokoni,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kuziongezea nguvu mamlaka hizi kwa kuzipatia rasilimali fedha na watu ili iweze kuimarisha ukaguzi wake nchi nzima. Vile vile kwa watendaji wanaojihusisha na vitendo vya rushwa wachukuliwe hatua stahiki ili kukomesha vitendo hivyo.

### **3.1.9 Vibali vya kuingiza Sukari Nchini**

**KWA KUWA**, vibali vya kuingiza sukari vimekuwa vikitolewa bila kuzingatia *Gap Sugar* iliyopo kwa wakati husika jambo linalotoa mianya kwa wafanyabiashara wasio waaminifu kuamua kupunguza uzalishaji na kuingiza sukari zaidi kutoka nje ya nchi,

**KWA KUWA**, hatua ya kupunguza uzalishaji inamadhara katika ajira,

**HIVYO BASI**, Bunge linaishauri Serikali kabla ya kutoa vibali kwa mwaka 2019 ifanye tathimini upya kwa lengo la kubaini uwezo wa viwanda vya ndani na *Gap Sugar*, hatua ambayo itasaidia kubaini mahitaji halisi lakini pia kujua sifa za waombaji na kuondoa hali ya sintofahamu inayoendelea sasa.

### **3.1.10 Changamoto za Baraza Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**KWA KUWA** Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira limepewa majukumu ya kisheria ya kusimamia masuala ya kuhifadhi mazingira

**NA KWA KUWA** Baraza limekuwa likishindwa kutekeleza majukumu yake kiufanisi kutokana na ufinyu wa rasiliamali fedha, kukosa wataalamu wenye taaluma ya mazingira na kukosa vitendea kazi,

**HIVYO BASI** Bunge linaishauri Serikali kuzingatia madhumuni ya kuanzishwa kwa chombo hiki

### **3.1.11 Ufinyu wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira**

**KWA KUWA** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira imepewa jukumu kubwa la kuratibu na kusimamia masuala yote uhifadhi wa mazingira hapa nchini,

**NA KWA KUWA** upatikanaji wa fedha ndio nguzo ya kupata matokeo yaliyokusudiwa

**HIVYO BASI** Bunge linaishauri Serikali kutenge Bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza jukumu ya uhifadhi wa mazingira.



### **3.1.12 Tozo za Mazingira kuingizwa katika Mfuko wa Mazingira**

**KWA KUWA** mfuko wa Mazingira ulianzishwa kwa madhumuni ya kuisaidia wizara yenye dhamana ya Kusimamia masuala ya mazingira kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi,

**NA KWA KUWA** tumeshuhudia hali ya utengaji fedha kwa ajili ya Uhifadhi na Usimamizi wa Maizngira sio wa kuridhisha,

**NA KWA KUWA** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira ilikwisha kamilisha mapendekezo ya vyanzo vya mapato na viwango vya uchangiaji kwa sekta nyingine katika Mfuko wa Mazingira na kuviwasilisha Serikalini.

**HIVYO BASI,** Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 vyanzo vya mapato vya Mfuko wa Mazingira ambavyo vimeainishwa na kuwasilishwa Serikalini vinapata kibali na kuanza kuchangia katika Mfuko huu kwa lengo la kuuwezesha kufanya kazi yake iliyokusudiwa.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe kwa uongozi wako uliotukuka na kwa ushirikiano ambao umekuwa ukiipatia Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake. Na pia, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kuanzia Machi 2018 hadi kufikia Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa **Mheshimiwa John Pombe Magufuli**, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hatua na juhudi mbalimbali anazozionyesha tena kwa vitendo katika kuhakikisha **Azma ya Kujenga Tanzania ya Viwanda** inafanikiwa. Kamati inaunga mkono juhudi zake na itaendelea kuisimamia na kuishauri Serikali kuhakikisha kwa pamoja tunafanikisha azma hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano walioutoa katika kuandaa taarifa hii mpaka kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo;-

i.	Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb	<b>Mwenyekiti</b>
ii.	Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb	<b>M/Mwenyekiti</b>
iii.	Mhe. David Cecil Mwambe, Mb	Mjumbe
iv.	Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb	Mjumbe
v.	Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb	Mjumbe
vi.	Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb	Mjumbe
vii.	Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb	Mjumbe
viii.	Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb	Mjumbe
ix.	Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb	Mjumbe
x.	Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb	Mjumbe
xi.	Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb	Mjumbe

xii. Mhe. Kmamis Ali Vuai, Mb	Mjumbe
xiii. Mhe. Zainab Mdolwa Amiri, Mb	Mjumbe
xiv. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb	Mjumbe
xv. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb	Mjumbe
xvi. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb	Mjumbe
xvii. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb	Mjumbe
xviii. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb	Mjumbe
xix. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb	Mjumbe
xx. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb	Mjumbe
xxi. Mhe. Machano Othman Said, Mb	Mjumbe
xxii. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb	Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote wa Wizara zilizochini ya usimamizi wa Kamati, pamoja na Makatibu Wakuu, Watendaji wote wa Wizara na Taasisi chini ya Wizara kwa ushirikiano walioipa Kamati kwa kufika mbele ya Kamati na kutoa ufafanuzi mara walipohitajika.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati na kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu kiukamilifu. Pamoja na yeye, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Wilfred Magova na Bi. Zainab Mkamba pamoja na wasaidizi wa Kamati Ndg. Modester Kipiko, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali **maoni**, **ushauri** na **mapendekezo** ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

.....  
Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA VIWANDA,**  
**BIASHARA NA MAZINGIRA**  
4 Februari, 2019